SportPesa
TZS. 517,350,800
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Bomoabomoa** vibanda vya machinga yarindima usiku Dar es Salaam

UKURASA 3



**Solskjaer: Sijutii kuondolewa EFL**

UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Septemba 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580713

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUM

# Serikali yakiri tatizo kesi ya Rugemalira

UKURASA 4







Baadhi ya wafanyabiashara wadogo waliokuwa wanafanya shughuli zao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam, wakilinda na wengine kuhamisha mabaki ya bidhaa na vibanda vyao, vilivyobomolewa na askari wa Jiji hilo usiku wa kuamkia jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Polisi, Msajili wabaini tatizo kisheria kuzuia vikao vya ndani

UKURASA 2

## Bosi: Sabaya hakuruhusiwa kutekeleza majukumu ya nje

UKURASA 3

**MICHEZO** BIASHARA UTD HAIWAOGOPI YANGA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza kwenye mkutano wa pamoja kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na Marekani, jijini New York, nchini Marekani juzi. **PICHA: IKULU**

# Samia ateta na bosi EU na wafanyabiashara Marekani

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameshiriki mkutano wa pamoja kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na Marekani na kuhimiza kuimarishwa kwa biashara kati ya mataifa hayo mawili ili kuwa na faida kwa pande zote.

Katika mkutano huo uliofanyika jana, Rais aliwaeleza wafanyabiashara hao kuwa kwa sasa biashara zinazofanyika kati ya Tanzania na Marekani ni ndogo kulinganishwa na fursa zilizopo.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2019, Tanzania iliagiza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 241 na kuuza bidhaa zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 46.

Kwa upande mwingine, Marekani imewekeza Tanzania Dola za Kimarekani bilioni 5.55 na kuajiri watu 44,118 wakati Tanzania imewekeza kiasi cha Dola za Kimarekani milioni moja tu ambacho ni kidogo kulinganishwa na ukubwa wa uchumi wa Marekani duniani na fursa zilizopo nchini.

Rais Samia aliwaeleza wafanyabiashara hao kuwa angependa kuona biashara inaongezeka kwa kuwa Tanzania ni mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki(EAC) na pia Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambazo zinatoa fursa za wawekezaji na wafanyabiashara wa Marekani kwa soko la watu milioni 450, hivyo kuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Vilevile, aliwaeleza wafanyabiashara hao kuwa Tanzania imetia saini mkataba wa Biashara Huru Barani Afrika (AfCFTA) ambao umelegeza masharti ya biashara na kuunganisha soko la watu bilioni 1.3.

Rais Samia pia alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya (EU), Charles Michel, ambaye alimshukuru mkuu wa nchi huyo kwa kukutana naye na kueleza kuwa lengo lake ni kutaka kupata maoni ya Rais Samia kuhusu mambo manne ya kipaumbele kwa Umoja wa Ulaya kwenye uhusiano wake na Afrika na utayari wa Umoja wa Ulaya kushirikiana na Tanzania kwenye maeneo hayo.

Mambo hayo ni UVIKO-19, Mabadiliko ya Tabia Nchi, Hali ya Usalama Msumbiji na Mapinduzi ya Kidijitali.

Rais Samia aliushukuru Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano wake na kuelezea hatua ambazo Tanzania inachukua katika kukabiliana na UVIKO-19, hasa ikizingatiwa kuwa ugonjwa huo umeathiri sekta nyingi ikiwamo ya utalii.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia alieleza hatua mbalimbali ambazo serikali inachukua katika kusambaza miundombinu ya afya ingawa bado kuna vikwazo katika upatikanaji wa vifaa tiba na rasilimali watu na hivyo kuukaribisha Umoja wa Ulaya kuangalia namna ya kushirikiana na Tanzania katika maeneo hayo.

Kuhusu mabadiliko ya tabia nchi, Rais Samia alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoathirika na mabadiliko hayo na inalipa kipaumbele suala hilo katika kukabiliana nalo.

Rais Samia pia alihudhuria mkutano wa kuadhimisha miaka 20 ya tamko la Durban kuhusu kupinga ubaguzi wa rangi na aina zote za unyanyasaji.

Leo Rais Samia anatarajiwa kuhutubia Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa unaoendelea New York, Marekani.

# Wafanyabiashara wakubwa walipa mabilioni kodi TRA

**Na Romana Mallya**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Alphayo Kidata, amesema katika kipindi cha miezi miwili iliyopita (Julai na Agosti) Idara ya Walipakodi Wakubwa imekusanya mapato ya kodi ya Sh. trilioni 1.152.

Kidata alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam katika kikao baina yake na walipakodi wakubwa kilichojumuisha watafiti na wachimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia, wasambazaji wa mafuta na vilainishi, wazalishaji wa nishati, washauri wa kodi na washauri elekezi.

Kidata alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, TRA ilikusanya jumla ya Sh. trilioni 18.148 ambapo Idara ya Walipakodi Wakubwa ilikusanya Sh. trilioni 6.879 ikiwa ni takribani asilimia 38 ya makusanyo yote. Alisema kwa mwaka huu wa fedha, TRA imepewa jukumu la kukusanya Sh. trilioni 22.3 na kwa Idara ya Walipakodi Wakubwa imepangwa kukusanya Sh. trilioni 9.5.

"Ni matarajio yetu kama ambavyo imekuwa desturi yenu, mtaiwezesha mamlaka kukusanya kiasi hiki cha fedha kwa hiari na pasipo udanganyifu," alisema.

Pia alisema ritani za kodi zinakaribia Sh. trilioni moja na kwa miezi minne kuanzia Mei wamelipa zaidi ya Sh. bilioni 300 na mwezi huu wanatarajia kulipa Sh. bilioni 270 na matarajio ni kabla ya kuisha mwaka huu wa fedha wawe wamemaliza.

Kidata alisema lengo la kikao hicho ni kuwasikiliza na kujadiliana na wafanyabiashara na mambo mbalimbali yatakayosaidia kuboresha utendaji wa TRA.

Kidata alitumia kikao hicho kuwakumbusha wafanyabiashara hao kulipa kodi kwa hiari na kuwaeleza kuwa hawapendi kutumia nguvu katika usimamizi wa kodi.

# Polisi, Msajili wabaini tatizo kisheria kuzuia vikao siasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi nchini limekutana na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini kujadili masuala mbalimbali, huku wakibainisha kuwapo kwa shida ya kisheria kwenye vikao vya ndani vya vyama vya siasa.

Kikao hicho kilifanyika jana jijini hapa ambapo Mkuu wa Jeshi hilo (IGP), Simon Sirro, alisema wamekutana kujadili vikwazo vilivyokuwa vinajitokeza kwenye baadhi ya vyama vya siasa kwenye mikutano yao ya ndani na nje ambayo wamekuwa wakizuia.

"Kimsingi tumezungumza na kuona kweli kwenye mikutano yao ya nje hakuna shida na si vyama vingi vinavyolalamika kuwa tumekuwa tunaingilia, lakini shida kubwa ipo kwenye mikutano ya ndani na tumeona upande wa sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi wasaidizi na sheria ya vyama vya siasa havijatamka bayana kuhusu sheria inayotawala vikao vya ndani vya vyama."

"Kumekuwapo na mwingiliano au sintofahamu kwa maana kwamba baadhi ya vyama vya siasa mkutano badala ya kuufanyia nje wanakuja kuufanyia ndani na wanapofanyia ndani mikutano ya nje mara nyingi lazima tuambiwe ajenda za mkutano huo ni kitu gani... kwa changamoto hiyo inaonekana kuna ombwe la kutokuwa na sheria ambayo inayoelezea mikutano ya ndani maana yake nini na sheria inayotawala mikutano ya ndani ya namna gani," alisema.

Alishauri Msajili wa Vyama vya Siasa kulizungumzia hilo na wanasiasa ili polisi ambao ni wasimamisizi wa sheria waone uelekeo.

"Lakini jambo kubwa katika mikutano yote miwili ya hadhara na ya ndani sisi Jeshi la Polisi tunaangalia usalama kwanza, tunaangalia suala la amani na utulivu katika hiyo mikutano tukiangalia suala la amani na utulivu ni changamoto au kuna tishio lolote la amani na utulivu basi ni lazima tuchukue hatua kwasababu ni kazi yetu ya msingi."

"Lakini jingine tulichoona suala la kukata rufani kwa waziri pale ambapo OCD ametoa angalizo au amekataa kile kikao au mkutano usiendelee basi ni vizuri akawashauri viongozi wa kisiasa kuona watumie ile forum ya kuweza kukata rufani kwa waziri ili waziri aweze kubatilisha maamuzi ya OCD au kuona kwamba maamuzi ya OCD ni sahihi," alisema.

Hata hivyo, alisema wamekubaliana kuna kila sababu ya jeshi hilo kuwa karibu na viongozi wa vyama vya siasa kwa kuwa ni wadau muhimu katika suala la ulinzi na usalama.

"Tumekubaliana mambo mengi ya kufanya kuhakikisha mwisho wa siku nchi yetu inakuwa ya amani na utulivu. Niwaombe kwa sababu msajili wana kikao cha kukutana na wanasiasa niwaombe basi ni vizuri na sisi tukapata taarifa kwa kuwa lengo ukipata taarifa unaitumia taarifa ili mwisho wa siku ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na amani na utulivu," alisema.

Naye Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alisema kikao hicho mchakato wa vikao vya awali kabla ya kufanya kikao cha wadau Oktoba 21, mwaka huu. "Sikupenda kusubiri nifanye kikao moja kwa moja cha wadau kabla ya wahusika wakuu wa suala hili ambalo tulikuwa tunalifuatilia kukaa nao. Nashukuru tumepata ushirikiano mzuri na tumeongea mambo mengi ambayo na mimi yamenifungua macho kwamba tumekuwa tukifanya kazi lakini cha msingi nilichojifunza mawasiliano ya mara kwa mara kwenye hizi taasisi ni muhimu," alisema.

Aliongeza: "Nitawaeleza wanasiasa mambo yaliyoelezwa, lakini kikubwa tunataka kupunguza misuguano ambayo haina ulazima... leo nimegundua kwamba kuna mambo ambayo hatuyajui sisi, lakini wangekuwa kila kitu wanakieleza tungejua tunafanya siasa au wakati mwingine tunafanya fujo, kwa hiyo tutafikisha kwa wadau wa siasa ili kuwa na mwelekeo mzuri."

## HABARI KITAIFA

# Bosi: Sabaya hakuruhusiwa kutekeleza majukumu ya nje

**Na Allan Isack,ARUSHA**

KATIBU Tawala Msaidizi wa zamani wa Mkoa wa Kilimanjaro, Renatus Msangira (45), amependa kizimbani, akidai aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani humo, Lengai Ole Sabaya, hakupewa kibali chochote cha maandishi kwenda kutekeleza majukumu nje ya kituo chake cha kazi.

Msangira, ambaye ni shahidi wa kwanza wa upande wa Jamhuri, alitoa madai hayo jana, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha wakati akitoa ushahidi wake, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Filex Kwetukia.

Sabaya na wenzake sita, wanakabiliwa na mashtaka matano, ya matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Washtakiwa wenzake katika shauri hilo la uhujumu ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Mbele ya Hakimu wa mahakama hiyo, Patricia Kisinda, alidai Sabaya hakuwahi kupewa kibali cha maandishi kwenda kutekeleza majukumu nje ya kituo chake cha kazi cha Wilaya ya Hai.

Alidai kiutaratibu Mkuu wa Wilaya akitaka kwenda kufanya kazi nje ya kituo chake cha kazi inatakiwa apate kibali cha maandishi kutoka kwa Mkuu wa Mkoa, lakini hilo halikufanyika.

"Kwa kuwa mimi nilikuwa RAS Msaidizi ninayesimamia utawala na rasilimali watu katika Mkoa wa Kilimanjaro, kama Sabaya angekuwa amepewa kibali cha maandishi na RC kwenda kufanya kazi nje ya wilaya yake ningefahamu kwa kuwa kingepitia kwenye ofisi yangu kwa kuwa mimi ni msimamizi wa shughuli za kiutawala," alidai shahidi huyo.

Msangira, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia utawala na mipango katika Wizara ya Fedha na Mipango, alidai kwamba awali alikuwa mtumishi katika Mkoa wa Kilimanjaro, kuanzia Machi 20, mwaka 2020 hadi Juni mwaka huo ndipo akahamishwa kupelekwa wizarani.

"Katika mazingira ya kawaida DC akitaka kutoka nje ya kituo chake cha kazi kwenda sehemu ya wilaya nyingine au mkoa mwingine kwenda kutekeleza majukumu ya kikazi, lazima aombe ruhusa kwa kiongozi wake wa Mkoa na apewa kibali cha maandishi,'"alidai.

Alidai katika kipindi cha Machi hadi Juni mwaka huu, Sabaya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, lakini Mei 13, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alimsimamisha kazi kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zilizokuwa zikimkabili.

Katika hatua nyingine shahidi huyo, alidai kwamba Mkuu wa Wilaya hapaswi kuwa na walinzi binafsi kwa kuwa anakuwa na ulinzi wa askari polisi akiwa kazini, nyumbani kwake na kwenye ziara za kikazi kulingana jeografia ya eneo husika.

"Kwa utaratibu wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa, mawaziri na manaibu waziri hawatakiwi kuwa na walinzi binafsi lakini kama kuna jambo la kuhatarisha usalama wake anaomba kibali kutoka katika mamlaka husika za usalama.

Aliieleza mahakama kwamba endapo Mkuu wa Wilaya atahitaji kuwa na walinzi binafsi tenda itatangazwa na mshindi ndiye atapatiwa shughuli ya kutoa huduma hiyo.

"Ulinzi wa kwenye makazi wanalinda askari polisi na kama DC anahitaji walinzi binafsi Katibu Tawala wa Wilaya (DAS), anaandika barua kwa Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD),kuomba kuongewa walinzi binafsi kama wanahitajika.

# Bomoabomoa vibanda vya machinga yarindima usiku

**Na Romana Mallya**

AGIZO la Rais Samia Suluhu Hassan kwa wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuwapanga vyema wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, limeanza kutekelezwa jijini Dar es Salaam kwa kuondoa vibanda vilivyopo maeneo ya karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliagiza vibanda vya biashara vilivyoko pembezoni mwa barabara viondolewe.

Katika kutekeleza agizo hilo, jana Nipashe ilishuhudiwa vibanda vilivyokuwa maeneo ya kuanzia uwanja huo wa ndege hadi TAZARA vikiwa vimebolewa, mashuhuda wakidai kuwa ubomoaji ulifanyika usiku wa kuamkia jana.

Nipashe ilishuhudia baadhi ya wafanyabiashara wakiwa wanachukua baadhi ya bidhaa zao zilizoharibiwa katika utekelezaji wa agizo hilo.

Septemba 13, mwaka huu, Rais Samia aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuchukua hatua za kuwapanga vyema machinga na kwamba hataki kuona anayoona kwenye televisheni ya kupigana, kuchafuana na vitu kumwagwa.

Wakati Rais akitoa agizo hilo, Septemba 9 mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Makalla alikuwa ameshapiga marufuku ufanyaji wa biashara kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara zote za mkoa huo baada ya utaratibu huo kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani na ongezeko la ajali.

Rais Samia aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya wakati wanachukua hatua ya kuwapanga machinga, wahakikishe hawasababishi vurugu, fujo na uonevu na kuwataka machinga nao wafuate sheria na kanuni zilizopo na kutii wanayopangiwa na viongozi hao wakiwamo wa wakuu wa wilaya.

Akizungumza katika Soko la Kariakoo, Makalla ambaye alilitembelea baada ya kuzuka ugomvi wa wafanyabiashara na mmoja wao kuvua nguo zote wakati wakigombea maeneo ya biashara, aliwaagiza wakuu wa wilaya kuainisha maeneo ambako watawapeleka.

Makalla alisema uchunguzi umebaini kuwapo kwa kero zinazosababishwa na ufanyaji biashara holela kwenye maeneo ya watembea kwa miguu na hifadhi za barabara.

# Rais Mwinyi azindua vitambulisho vya wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezindua vitambulisho vya wajasiriamali vitakavyosaidia kurasimisha shughuli zao na kuwatambua kisheria kuwa ni miongoni mwa wachangiaji wa uchumi.

Dk. Mwinyi alisema kuwa mbali ya hatua hizo pia, kuwapo kwa vitambulisho hivyo kutawarahisishia wajasiriamali hao huduma mbalimbali zikiwamo za kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

"Kwa hakika leo ni siku ya furaha kubwa kwangu kuona kuwa tumeweza kuitekeleza ahadi tuliyoitoa kwa wananchi na hasa wajasiriamali wadogo hapa Zanzibar ya kuwapatia vitambulisho maalum na vya kisasa," alisema Rais Dk. Mwinyi.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa pamoja na kuzingatia matakwa ya sheria mbalimbali zinazohusiana na wajasiriamali ikiwamo Sheria Namba Saba ya mwaka 2014, ikiwa na lengo la kuweka mazingira maalum ya kuyasaidia makundi ya wajasiriamali wakiwamo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Pia, alisema malengo ya serikali ni kutoa Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali na serikali itatoa Sh. bilioni 50 na benki zilizoamua kuwasaidia zitatoa Sh. bilioni 50 ambazo zitatumika kwa kuwatafutia mafunzo, mitaji pamoja na masoko.

Alisema tayari serikali imeshaanza mazungumzo na wawekezaji katika kufanikisha ujenzi wa masoko kwa kila wilaya Unguja na Pemba, huku akitoa taarifa katika kipindi kifupi kijacho serikali itaanza ujenzi wa masoko katika eneo la Jumbi na Chuini kwa Nyanya.

Aidha, alisema serikali ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo ya ujenzi katika eneo la Darajani ambalo litakuwa na sura mpya na fursa nyingi zaidi kwa wafanyabiashara wadogo kufanya kwa ufanisi.

Aliwapongeza wajasiriamali wote waliojitokeza kujisajili tangu zoezi hilo lilipoanza na kuwahimiza ambao hawajajisajili kufanya hivyo katika vituo vilivyoandaliwa.

Aliupongeza uongozi na watendaji wa Kampuni ya AIM Group Limited kutoka Dar es Saalam kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa mfumo wa usajili wa wajasiriamali wadogo Zanzibar uliozinduliwa rasmi jana na kuwawezesha kupata vitambulisho vyenye ubora.

Kwa upande wao wajasiriamali waliofika katika uzinduzi huo wamepongeza hatua hiyo ambayo itawarahisishia kufanya biashara zao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Idrissa Kitwana, alisema watajitahidi kusimamia zoezi hilo kwa uadilifu ili kufikia lengo lililokusudiwa la kuwasaidia wajasiriamali.


## TANGAZO LA MNADA
## GARI AINA YA MITSUBISH FUSO
### YENYE NAMBA ZA USAJILI T323 CFZ




116474302

**MNADA UNAFANYIKA KATIKA YARD YA KAMPUNI YA ADVANCED CREDIT ILIYOKO SAKINA KWA IDDI OPPOSITE LUSH GARDEN HOTEL.**

**TAR: 25/09/2021 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI**

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia 25% ya bei hapo hapo na asilimia 75 iliyobaki italipwa ndani ya siku 14.
2. Ukaguzi wa gari utafanyika siku mbili kabla ya mnada

Endapo mshindi atashindwa kulipa asilimia 75 iliyobaki ndani ya muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake na gari itauzwa upya

**Mawasiliano: 0785 132 130**

# Serikali yakiri tatizo kesi ya Rugemalira

Na Sanula Athanas

- Waziri ataja shida kisheria, amtetea DPP
- Gerezani: Wafungwa 52%; mahabusi 48%

**KATIKA sehemu ya kwanza jana, kuliainishwa madai yaliyopo kuhusu walakini wa upelelezi kisheria na mazingira yake. Endelea kufuatilia uchambuzi wa hoja hiyo, ikioanishwa na nafasi zingine za kisheria zinazogusa kasoro hiyo:**

Katika hoja yake, Mwanasheria Alloyce Komba anafungamana na kinachopaziwa sauti na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), akianzia na eneo la upelelezi ambalo anawasilisha hoja yake ya msingi kwamba: "Tunataka upelelezi wa kesi zote za Uhujumu Uchumi na kesi zingine uwe na ukomo."

Anaendelea: "Hii itapunguza mwenendo wa watu kushikiliwa mahabusu kwa muda mrefu kwa kisingizio kwamba upelelezi haujakamilika."

Komba pia anadai madaraka ya DPP yamepitiliza, hivyo yanapaswa kupunguzwa ili kuondoa mianya anayodai inaweka rehani sehemu ya haki za kibinadamu.

Anafafanua kwamba DPP anachukua nguvu ya mahakama, akirejea mifano hai ya kesi za Uhujumu Uchumi zinazotakiwa kusikilizwa na Mahakama Kuu, lakini zinapokuwa makahama za wilaya au mkoa zinahitaji kibali chake.

Mwanasheria huyo mwenye mzizi wa kutumikia Sekta ya Habari na sasa wakili wa kujitegemea, anafafanuzi kwamba mashtaka ya jinai hayapaswi kukinzana na Katiba ya nchi.

Hata hivyo, katika maoni yake ya kitaalamu huku akirejea baadhi ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, anadai mwenendo wa kesi iliyomhusu Rugemalira ulikiuka sheria hiyo kuu.

Wakili Benedict Ishabakaki ana dai la kukosoa taratibu za upelelezi nchini, akitaka ufanyike mapema na hatua za kujiridhisha zifikiwe na mamlaka za kisheria, ndipo shauri lihamie kwenye utaratibu wa kufikishwa mahakamani.

Huku akitoa mfano anaoueleza katika sura ya walakini unaoshuhudiwa kwenye shauri linalomhusu Mzee Rugemalira, wakili huyo anafafanua:

"Mtu akikamatwa wakati ushahidi haujakamilika, matatizo yake ndiyo kama haya yaliyotokea kwa Rugemalira, mtu anakaa mahabusu miaka minne ila hamna kitu chochote walichokikuta kwenye kesi yake."

**KAULI YA SERIKALI**

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda (pichani), alipotakiwa na Nipashe kutoa neno kuhusiana na sauti hizo kutoka kwa wanasheria wenzake, kwanza alikiri ukweli unaolalamikiwa wa kilio cha kesi kuchelewa mahakamani.

Hata hivyo, anasogeza kando lawama za kuchelewesha kesi kwa wadau wenza kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Rais (Utawala Bora) penye mzizi wa mashauri.

Pinda anafafanua: "Kesi ni jambo mtambuka, kuna TAKUKURU, Polisi, wote hao ni wapelelezi. Wakitoka hao anaingia DPP, yeye anajiridhisha kama kesi inastahili kusikilizwa mahakamani na kama ina maslahi makubwa zaidi, Wakili Mkuu wa Serikali anaingia.

"Hivi vyote vinafanyiwa kazi kila kimoja kwa wakati wake na tukumbuke kesi zinatofautiana uzito. Unaposema kuchelewa kwa kesi, lazima ujue kwanza sura ya kesi husika.

"Mahakama katika sura ya kawaida inaonekana kama ndiko mahali kesi zinakocheleweshwa, lakini ukweli ni kwamba mahakama haihusiki na upelelezi.

"Jaji au hakimu akiambiwa upelelezi umekamilika, anapanga tarehe ya kusikiliza ushahidi na baadaye hukumu. Tumejitahidi sana kupunguza msongamano wa kesi, mkakati wetu ni mzuri na kesi sasa zinakwenda kwa haraka."

Anasema hatua inayochukuliwa hivi sasa, wamepeana wito kwa wizara na vitengo vyote wadau wa kesi kuharakisha hatua za upelelezi kukiwapo muda maalum.

"Tumeweka malengo kesi za kawaida uchunguzi usizidi siku 60 na hizi kesi kubwa usizidi miezi sita. Tumejitahidi sana kuhakikisha kesi zinaamuliwa haraka," anafafanua hatua inayochukuliwa, akiwa na angalizo kuwa mashauri makubwa upelelezi unaweza kuvuka ukomo.Nini kilichojiri kisheria kwenye shauri linalolalamikiwa sasa linalomhusu Rugemalira na wenzake? Ni swali ambalo Nipashe inataka ufafanuzi kutoka kwa kiongozi huyo wa serikali.

Naibu Waziri katika majibu yake, anaeleza: "Kesi ya Rugemalira iliangukia kwenye Uhujumu Uchumi na mazingira ya uhujumu yanachukua muda mrefu kufanya utafiti wa kujiridhisha.

"Hawa walifika hadi hatua ya kukubaliana na DPP kulipa. Sasa inawezekana pande zote mbili zilikuwa zinavutana kwenye hilo."

Pinda ambaye katika majibu yake kwa Nipashe, yanavaa sura tatu; nafasi ya kiutawala, uanasheria na mwananchi wa kawaida, anaungana moja kwa moja na walalamikaji wanasheria wenzake na umma kuhusu madhara ya mtu kukaa muda mrefu mahabusu.

Akitumia mfano rejea wa mshtakiwa Rugemalira, Naibu Waziri huyo anaweka ujumbe wa simanzi yake binafsi, akisema kilichomfika Rugemalira na kwa namna hiyo akiwanyoshea kidole wote waliokaa muda mrefu mahabusu katika mazingira yanayofanana na hayo, hayana jema hata kidogo.

Ni darasa la kisosholojia analozama nalo, akisema laiti inapomwangukia mwenye umri wa ujana, si ajabu pakashuhudiwa mabadiliko makubwa kwa hali ya kifamilia aliyoiacha nyumbani, tukio litakalombebesha simanzi mpya ya kijamii hadi kiuchumi, ambayo matokeo yake ni kitendawili.

Hata hivyo, udadisi wa Nipashe kuhusu madaraka ya DPP, Pinda anarejea katika nafasi yake ya kisheria, akiukosoa mtazamo wa wanasheria wenzake kuwa ni ushauri uliokosa mbadala thabiti.

Anahoji: "Mamlaka ya DPP yapunguzwe, yapelekwe wapi? Kipande cha mamlaka yale kiende kwa nani? Polisi au TAKUKURU? Hayo ni mamlaka ambayo tumempa kisheria!"

**WAFUNGWA, MAHABUSI**

Rais Samia Suluhu Hassan alipozungumza katika ufunguzi wa kikao kazi cha maofisa Jeshi la Polisi mkoani Dar es Salam tarehe 25, mwezi uliopita, pia alitoa angalizo binafsi, akiona ukakasi wa ziada ya mahabusi katika mazingira yanayokosa hoja nzito.

Katika hilo, Rais alitoa maelekezo kadhaa ya kuondoa tatizo hilo, ikiwamo Jeshi la Polisi kuona namna ya kukaa na wadau wake wa sheria, kuangalia uwezekano wa kurekebisha sheria inayohusu mahabusi.

Rais alikemea ucheleweshaji upelelezi unavyoibebesha mzigo mkubwa serikali kuwahudumia watu walioko mahabusu kwa muda mrefu.

Katika hotuba hiyo ya Rais iliyobeba angalizo la kitaalamu, aliainisha takwimu hadi tarehe 23 ya mwezi uliopita, kulikuwapo mahabusi 15,194 huku wafungwa wakiwa 16,542, hali inayokaribia kufanana.

"Mahabusi hawa wapo waliokaa wiki, miaka miwili, miaka mitatu, mwaka mmoja na muda mbalimbali na wanalishwa na serikali," Rais Samia alisema na kuhimiza kesi zenye ushahidi dhaifu zinapaswa kufutwa na kuwarejeshea watuhumiwa uhuru wao.



**15,194**

**Idadi ya mahabusi kwenye magereza yote nchini hadi Agosti 23 mwaka huu.**

**16,542**

**Idadi ya wafungwa kwenye magereza yote nchini hadi Agosti 23 mwaka huu.**

HABARI KITAIFA

# Bomba la mafuta kulipa fidia bil. 25/-

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

MRADI wa Bomba la Mafuta Ghafi (EACOP), kutoka Uganda hadi jijini Tanga unatarajia kutumia Sh. bilioni 25 kuwalipa fidia wananchi watakaopitiwa na bomba hilo ili kupisha ujenzi wake.

Bomba hilo linapita katika mikoa nane iliyopo Tanzania, wilaya 24, kata 134 na utandazaji wake chini ya ardhi utachukua kilometa 1,443 kutoka nchini Uganda hadi mkoani Tanga.

Hayo yalisemwa jana jijini Mwanza na Ofisa wa Mazingira Mwandamizi kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Anamaria Simon, alipozungumza na wafanyabiashara wa Wilaya ya Kahama mkoani Shimyanga juu ya fursa ambazo zitakuwa rafiki kwao wakati wa ujenzi wa mradi huo.

Simon alisema katika Wilaya ya Kahama bomba hilo litapita kwa umbali wa kilometa 54, na kwamba wafanyabiashara wanaweza kupata fursa ya kuangalia mazingira mazuri ya kufanya shughuli za ujasiriamali katika eneo husika.

Alisema kuwa bomba hilo lina uwezo wa kusafirisha jumla ya mapipa 216,000 kwa siku, huku ujenzi wake ukigharimu kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 3.5 sawa na Sh. trilioni nane.

Akizungumza kuhusu EACOP,a mbaye ndiye mkandasani mkuu, Simon alisema kuwa kampuni hiyo inaundwa na kampuni nne ambazo zina hisa.

Katika hisa hizo TPDC na asilimia 15, kampuni ya Total kutoka Ufaransa asilimia 65, UNOC, asilimia 15 pamoja na kampuni ya CNOOC yenye asilimia 8.

Aidha, alisema kuwa katika kuelekea ujenzi wa mradi huo hatua iliyopo kwa sasa ni uchukuaji wa ardhi kutoka kwa wananchi, huku akiongeza kuwa bomba hilo litafanya kazi kwa miaka 25 na jumla ya wananchi 607 watalipwa fidia katika kata nane zilizopo katika Wilaya ya Kahama.

Mhandisi kutoka katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kutoka makao makuu Dodoma, Nyaso Makwaya, alisema kuwa kwa sasa ni bora kwa wamiliki wa kampuni ya wazawa kusajili kampuni zao ili waweze kupata fursa ya kufanya biashara na mradi huo.

Alisema kuwa hadi Agosti 31, mwaka 2021 jumla ya kampuni 852 zimesajiliwa na mamlaka hiyo na kuongeza kuwa kampuni hizo zimeagizwa kutumia bidhaa zinazotoka hapa hapa nchini.

# Biashara ya binadamu yawatupa jela miaka 140

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi imewahukumu kwenda jela miaka 140 watu watano, baada ya kukutwa na hatia ya kujihusisha na biashara ya kusafirisha ya binadamu kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya Lindi, Maria Batraine, baada ya washtakiwa wote kukiri makosa yaliyowakabiri.

Washtakiwa hao ni Issa Omari Magwila (37), Mohamedi Abdurahamani Jenga (40) wote wakiwa ni wakazi wa Vikindu, Mkoa wa Pwani.

Wengine ni Jafari Hamisi Mtanda (36), Ahmadi Khalfani Salum (38) wakazi wa Mtaa wa Majengo mkoani Mtwara na Juma Lupanga Wagondo (36) Mkazi wa Kijiji cha Mkunya Wilaya ya Newala mkoani Mtwara.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo washtakiwa walipewa nafasi ya kujitetea na kila mmoja kwa wakati wake waliiomba mahakama isiwape adhabu kali wakieleza kwamba ni mara yao ya kwanza kutenda kosa hilo, pia wanafamilia zinazowategemea.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batraine alimuuliza mwanasheria wa serikaili, Yahaya Gumbo, iwapo anazo kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washtakiwa na kujibu hapana, huku akiiomba mahakama iwape adhabu kali, ili iwe fundisho kwao na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

"Hakimu sina kumbukumbu zao, lakini naomba wapewe adhabu kali, ili kupunguza kama siyo kumaliza kabisa tabia hii haramu," alidai Gumbo.

Hakimu Batraine akitoa hukumu katika kesi hiyo ya jinai namba 52/2021, kupitia Sheria ya Uhamiaji kifungu cha 46 kifungu kidogo cha (1)(a), Sura ya 54 rejeo la 2016 na kifungu cha 46 kifungu kidogo cha (1) (1) (g) ya Sheria ya Uhamiaji sura ya 54 rejeo 2016.

Hivyo, Hakimu Batraine aliwahukumu mshtakiwa wa kwanza na pili kutumikia kifungo cha miaka 40 jela kila mmoja wakati mshtakiwa wa tatu, nne na tano kila mmoja alihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela, kufanya jumla ya miaka waliyofungwa kuwa 149.

Awali mahakamani hapo ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Yahaya Gumbo, kwamba washtakiwa wanajihusisha na mtandao wa kufanya biashara ya kusafirisha binadamu kinyume cha sheria.

Ilielezwa kwamba washtakiwa wote walikamatwa kwa nyakati tofauti wakisafirisha watoto wawili wenye umri wa miaka 12 raia wa Ethiopia.

Gumbo aliiambia mahakama hiyo kwamba watoto hao (Gidion Fantu na Mohamedi Egogo) walikamatwa Julai 18, mwaka huu, wakisafirishwa na washtakiwa hao kuelekea Afrika Kusini kinyume cha sheria.

Hata hivyo, watoto hao kwa sasa wapo chini ya uwangalizi wa Idara ya Ustawi wa Jamii mkoa, wakisubiri taratibu za kurejeshwa katika nchi yao.







Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe magonjwa yasiyoambukiza yanaangamiza

**NOVEMBA** 3 mpaka 6, mwaka huu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Taasisi ya Mpango wa Kupambana na Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), inaadhimisha Wiki ya Kupambana na Magonjwa Yasiyoambukiza, jijini Arusha.

Lengo la maadhimisho hayo ni kuwakumbusha na kuwahamasisha Watanzania umuhimu wa kuangalia afya zao mara kwa mara ili kujiepusha na athari za magonjwa hayo.

Magonjwa yasiyoambukiza ni yale yasiyo na vimelea vinavyoweza kusambazwa mfano magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, saratani, magonjwa sugu ya njia ya hewa, kisukari, kuoza meno, magonjwa ya akili na mengine ya kurithi kama selimundu.

Serikali inatumia gharama kubwa katika bajeti yake kutibu magonjwa yasiyoambukiza na kwa mwaka 1991 ilionyesha kuwa asilimia tisa ya bajeti ilitibu wagonjwa wa kisukari.

Kwa mujibu wa wataalamu wa TANCDA, magonjwa haya yanaongezeka kwa kasi na kuwaathiri hata watu wenye umri mdogo wakiwamo watoto.

Mwaka 2016, watu milioni 42 (sawa na asilimia 71 ya vifo vyote) walifariki duniani kutokana na magonjwa yasiyoambukiza.

Asilimia 75 ya vifo vyote vinavyohusu watu wenye miaka 30 -70 husababishwa na magonjwa hayo.

Sababu zinazoelezwa za kuongezeka kwa magonjwa hayo ni mabadiliko ya mtindo wa maisha ikiwamo kutofanya mazoezi, kukaa ofisini, darasani kwa muda mrefu, kuangalia runinga, kutumia lifti kupanda majengo ya ghorofa, kupanda magari na kutoshiriki michezo.

Sababu nyingine ya kuongezeka kwa magonjwa hayo ni ulaji usiofaa, kwa mfano kula chakula kuzidi mahitaji ya mwili na hivyo kunenepa, kula sukari, mafuta na chumvi zaidi ya mahitaji ya mwili, kutokula mboga na matunda kiasi cha kutosha, kula nafaka zilizokobolewa na kunywa juisi badala ya matunda yenyewe.

Wataalamu hao wanasema pia matumizi ya pombe, tumbaku na dawa za kulevya yanachangia magonjwa yasiyoambukiza, vile vile msongo wa mawazo na kutopata usingizi wa kutosha.


Ili kuepukana na magonjwa hayo inashauriwa kufanya mazoezi na kila mlo uwe na makundi yote matano ya vyakula ambayo (a) ni nafaka, mizizi, ndizi mbichi za kupika, (b) matunda, (c) mboga, (d) jamii ya mikunde na asili ya wanyama na (e) mafuta.

Chakula mchanganyiko humwezesha mtu kupata virutubishi vyote vinavyohitajika mwilini, ikiwamo wanga ambao husaidia kuupa mwili nguvu na joto. Vyakula vya protini husaidia kujenga mwili na kutengeneza vichocheo mbalimbali, vitamini na madini hulinda mwili dhidi ya magonjwa.

Wataalamu wanashauri kuwa mwili unahitaji nguvu kila dakika, hivyo ni vizuri kula kila njaa inapouma. Milo mitatu kwa siku, pamoja na asusa moja asubuhi na nyingine jioni. Kifungua kinywa ni muhimu kila asubuhi kwa kuwa mtu anapoamka akiba ya sukari mwilini huwa ndogo baada ya muda mrefu bila chakula.

Katika utafiti uliofanywa mwaka 2012 nchini ulioshirikisha watu wenye umri wa miaka 25 na kuendelea, kwa kila watu 14 waliokutwa na shinikizo la juu la damu, ni mmoja pekee kati yao ndiye aliyekuwa amegunduliwa tayari.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Malezi mtoto kila kukicha, dawa inayomfikisha salama

Na Paulina Chimeledya. Tudarco

**MALEZI** mara zote ni suala nyeti sana, hasa kwa malezi ya watoto wanaoanza kukua na hii ni pale tu mtoto anapoingia kwenye rika ya ukuaji, jambo linalomfanya kijana na hasa binti apate malezi sahihi, pia mvulana, inagawaje kwa watoto wa kike unahitaji unyeti wa kutosha.

Nitapenda kutambua na kutumia nafasi ya wazazi,walezi na jamii kwa ujumla, kuwapongeza kwa malezi bora wanayowapa watoto wa kike na wa kiume wakiwajenga kwenye maadili mema

Lakini, pamoja na kwamba wazazi wanapambana kumlinda na kumkumbusha mtoto maadili mema, bado ulinzi kwa watoto wa kike unahitaji kutiliwa mkazo wa kutosha.

Hii si nyumbani pekee, hata anapotoka nyumbani kuelekea shuleni na mitaani jama vile sokoni au anapoaga kuelekea kwa marafiki zake.

Nazungumza hili, kwa sababu watoto wengi wanapotoka nyumbani hawana uangalizi mkubwa. Ni hali ambayo inachangia wengi kutokufikia maeneo sahihi waliotakiwa na badala yake wanaishia kusimamishwa mitaani.

Hiyo ni hasa vichochoroni wakiwa na marafiki zao,vijana wengine wa mtaani na hata watu wazima. Vyote vinaangukia hatari kwa usalama wao .

Hilo limejitokeza katika mitaa mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na hata mikoani na ninaweza kusema kwamba, huenda ni kutokana na 'ubize' wanaokuwa nao wazazi katika majukumu yao, kiasi kutoka nje ya wanayopaswa.

Niseme hapo mahsusi ni kwa mazingira ambayo watoto wanatembelea, hali ambayo hawaelewi ni nini wanachofanya na wanakutana na kina nani.

**Hilo limejitokeza katika mitaa mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na hata mikoani na ninaweza kusema kwamba, huenda ni kutokana na 'ubize' wanaokuwa nao wazazi katika majukumu yao, kiasi kutoka nje ya wanayopaswa.**

Hali hiyo inaweza kuwa ya kawaida, lakini upande wa pili kuna hatari sana kwa watoto wa kike, kwani wasipoangaliwa kwa umakini stahiki, wanaweza kujikita kwenye tabia hasi kama vile kutofika shuleni.

Mengine ni kuacha kabisa shule, kuanzishaa uhusiano mapema na vijana wanaosimama nao vichochoroni, hali inayoangukia moja kwa moja hatari ya kutofikia malengo stahiki kwa mabinti wasichana hao.

Kwa mantiki hiyo, ni wito wangu na ushauri kwa wazazi na walezi kutilia mkazo suala la uangalizi kwa watoto hao punde tu anapotoka nyumbani kuelekea shuleni na maeneo mengine yanayomfanya akutane na jamii, ikiwa ni pamoja na kufatilia mienendo ya watoto hao wawaoo shuleni na hata wao mtaani.

Pia, ni vyema wazazi wakakemea mara moja wanapogundua mtoto anapokuwa marafiki wasio sahihi iwe ni wa rika lake au vinginevyo, itasaidia sana kutokomeza tabia inayomfanya asitimize ndoto zao.

Hapo ndipo rai yangi ni kwamba, jamii isimame kidete kuwalinda wasichana hao kwani siku zote malezi hujumuisha jamii, ikizingatiwa falsagfa ya "mtoto wa mwenzio ni wako.

Ni muhimu pale kila mmoja atakapohisi uchungu kumuona binti katika mazingira hatarishi.

Jambo hilo la kuingia kati mwenendo wake, ni msaada wa kumkumbusha mtoto huyo maadili na mwenendo anayoelezwa kila siku na wazazi wake ,walimu na hata watu wazima kwenye jamii yake, ambayo kwa ujumla inamrejesha kuimarika kijamii.




Baadhi ya wajasiariamali wanaowezeshwa na kampuni ya Barrick wakionyesha bidhaa mbalimbali wanazozalisha katika maonyesho ya wajasiriamali yaliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), yanayoendelea katika viwanja vya Umoja, wilayani Kasulu, mkoani Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango aagiza ubunifu wa teknolojia SIDO

**Kalebo Mussa na Ally Mlanzi, TUDARCo**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kulitathmini Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), katika ubunifu wa teknolojia na uendelevu wake kwa maendeleo ya sekta hiyo.

Akifungua maonyesho ya tatu ya SIDO, jana wilayani Kasulu mkoani Kigoma, alisema mchango wa viwanda vidogo katika uchumi ni mdogo, kwa kuwa baadhi ya bidhaa zinazotengezwa hazikidhi viwango vya soko.

"Ninaitaka wizara ifanye tathmini ya kina kuhusu SIDO imefanikiwa au imeshindwa kiasi gani katika kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake na kuja na mapendekezo, mikakati mpya itakayopelekea Tanzania kukidhi mahitaji ya uchumi wakati wa juu kwa upande wa uzalishaji wa mashine ndogo na kati, vipuri, bidhaa na kadhalika katika karne 21," alisema Dk. Mpango.

Awali, Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alisema atahakikisha Kigoma kunakuwa na kiwanda kikubwa cha kuzalisha mafuta ya mawese.

"Nawaomba wanaKigoma mtumie fursa ya kuwa na Makamu wa Rais kuanzisha kiwanda kingine kikubwa, hapa Kigoma tayari kuna zao la chikichi tupate kiwanda kikubwa cha kuchakata mafuta ya kula ya mawese," alisema.

Naye Meneja wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Magharibi, Bejamini Dotto, alisema: "Tunafurahi sana kujumuika na SIDO katika kuhakikisha kwamba ukuaji wa viwanda vidogo ni endelevu, unazingatia utunzaji na usimamizi wa mazingira, tupo tayari kuwahudumia popote pale panapohitajika."

# Vijana wajumuishwa vita dhidi ya rushwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Deogratius Ndejembi, amezindua mwongozo wa kufundishia vijana wa skauti ambao umelenga kuwa na vijana wanaoikataa rushwa.

Aidha, Ndejembi amewataka maofisa elimu wa mikoa kuhakikisha baada ya mafunzo hayo kukutana na maofisa wote wa Idara ya Elimu walio chini yao katika wilaya zote ili kufikisha elimu hiyo kwa ambao hawajaipata.

Akizungumza katika ufunguzi na uzinduzi wa mwongozo huo jana, Ndejembi alisema mafunzo yamekuwa yakitolewa kwa watu wachache ili nao wakafikishe ujumbe kwa walio chini yao, lakini haifanyiki hivyo.

"Natoa agizo na siyo ombi, nataka mtakaporudi kwenye maeneo yenu ya kazi mkakutane na walio chini yenu, tunataka elimu iliyopo katika mwongozo huu ikawafikie vijana kote nchini ili kufahamu elimu ya kupambana na masuala ya rushwa na hatimaye kuikataa rushwa kabisa," alisema Ndejembi.

Kwa mujibu wa Ndejembi, mwongozo huo ni hatua nzuri katika mapambano dhidi ya rushwa kwani baada ya kuelimishwa vijana, wataifahamu rushwa na watashiriki ipasavyo kukabiliana nayo na utajenga msingi imara wa kuichukia rushwa.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kumzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Neema Mwakalyelye, alisema mwongozo huo umelenga kutoa elimu ya masuala ya rushwa kuanzia shule za msingi na kuendelea kuweka misingi mizuri kwa vijana ya kuichukia rushwa tangu wakiwa wadogo.

Vilevile, alisema utawawezesha watendaji kuwa na maudhui ya kuwashirikisha vijana wa skauti katika mapambano dhidi ya rushwa.

"Mwongozo huu umeweka msisitizo kupambana na rushwa katika mitihani na katika uchaguzi na maeneo mengine...hii itasaidia kuwawezesha vijana kuona na kutambua viashiria vya rushwa na kutoa taarifa kwa mamlaka husika."

Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU, Dk. Emmanuel Kiyabo, alisema mafunzo hayo yamehusisha wadau mbalimbali wakiwamo Chama cha Skauti Tanzania, wakuu wa TAKUKURU wa mikoa na maofisa elimu wa mikoa ambao watapitishwa katika mwongozo huo ili nao wakautekeleze kwenye mikoa yao.

Skauti Mkuu Tanzania, Mwantumu Mahiza, alisema mwongozo huo utakuwa na tija kubwa kwani rushwa imeleta athari nyingi hasa kwa wananchi wanyonge na taifa kwa ujumla.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **DOLPHIN GENERAL BUSINESS ENTERPRISES CO. LTD, WAUNGWANA AUCTION MART, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTYMANAGERS CO. LTD, COPS AUCTION MART AND COURT BROKERS, CHAMPION AUCTION MART** kwa niaba ya **Access Microfinance Bank Tanzania Limited** watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MBEYA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES CO. LTD | MWAKYUSA/Z,FURAHA | MWAKYUSA/Z,FURAHA | NYUMBA | TUKUYU | 11/10/2021 |
| 2 | MBEYA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES CO. LTD | MZIHO/O,STEWARD | MZIHO/O,STEWARD | NYUMBA | MBEYA | 12/10/2021 |
| 3 | MBEYA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES CO. LTD | WASENGA/ADAM, GODWIN | HOYO/A,FREDY | NYUMBA | MBALIZI | 12/10/2021 |
| 4 | MBEYA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES CO. LTD | MWAIBOFU/A,DAUDI | MWAIBOFU/A,DAUDI | NYUMBA | MBEYA | 13/10/2021 |
| 5 | MBEYA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES CO. LTD | SIMCHIMBA/J,ZAINA | SIMCHIMBA/J,ZAINA | NYUMBA | MBEYA | 12/10/2021 |
| 6 | MBEYA | DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES CO. LTD | KASANGA/DAUDI, EMMANUEL | KASANGA/DAUDI, EMMANUEL | NYUMBA | NDAGA | 13/10/2021 |
| 7 | LUMUMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD | LYAKURWA/ELIAS, ANSILA | MOSHI/SIFAELI, WILKINS | NYUMBA | VISIGA KIBAHA | 11/10/2021 |
| 8 | KIJITONYAMA | COPS AUCTION MART AND COURT BROKERS | ISSEME/MALABA, FREDY | KOMBA/NATHAN, GRACE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | MBAGALA CHARAMBE - ZOMBOKO | 11/10/ 2021 |
| 9 | KIJITONYAMA | WAUNGWANA AUCTION MART | SANGA/LAMECK, JOVIN | SANGA/LAMECK, JOVIN | KIWANJA- KUHAWILISHA | PUGU - BANGULO | 11/10/2021 |
| 10 | PAMBA | CHAMPION AUCTION MART | CHACHA/WARIOBA, SANGARARA | CHACHA/WARIOBA, SANGARARA | MOTORVEHICLE TOYOTA WILLS REG NO T 485DEX | MWANZA | 04/10/2021 |
| 11 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | MAHANO/BENJAMINI, FIKIRI | MAHANO/BENJAMINI, FIKIRI | VIWANJA VIWILI VYENYE HATI MILIKI | KIMBIJI | 12/10/2021 |
| 12 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | ASSENGA/KANYINYI SIMON | ASSENGA/STEVEN, PRISCUS | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 115384 | KIBAMBA LUGURUNI | 11/10/2021 |
| 13 | LUMUMBA | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD & PROPERTY MANAGERS CO LTD | HAMIS/CHARLES, HAMIS | KUBOJA/B,BWIRE | NYUMBA | GOBA | 13/10/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa

**MAWASILIANO**
**WAUNGWANA AUCTION MART - 0713077474**
**DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES C. LTD - 0754448694**
**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD - 0754497396**
**COPS AUCTION MART AND COURT BROKERS - 0716884999**
**CHAMPION AUCTION MART - 0716070188**
**WOTE MNAKARIBISHWA**

116475302

# Vifo vya kinamama vyapungua Kanda ya Ziwa

**Na Patson Andugalile,** TUDARCo

IDADI ya vifo vya kinamama mikoa ya Kagera, Mara na Geita imepungua kutoka 231 mwaka 2016 hadi 170 mwaka 2020.

Aidha, Visiwani Zanzibar vimepungua katika hospitali zilizofadhiliwa kutoka 67 mwaka 2016 hadi 47 mwaka 2020.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini, huduma za uzazi wa mpango baada ya mama kujifungua zimeongezeka kwa asilimia 12 mwaka 2016/17 hadi 26 mwaka 2019/20.

Taarifa hiyo ilitolewa wakati wa maadhimisho ya miaka mitano ya kuboresha huduma ya malaria, afya ya uzazi, afya ya mama na mtoto na watoto wachanga, na vijana kupitia mradi wake wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa Boresha Afya, Kanda ya Ziwa na Nyanda ya Magharibi.

"Kuhakikisha kuwa wenza wanapata huduma bora za uzazi wa mpango baada ya kujifungua na kusaidia kupanga muda mwafaka wa kupata mtoto na ustawi wa afya ya mama na mtoto," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kinga dhidi ya malaria kwa wajawazito na watoto ambao hawajazaliwa kwa kutumia tiba kinga wakati wa ujauzito (IPTp3 +), na matumizi ya tiba kinga yameongezeka kutoka asilimia 28 mwaka 2016 hadi 66 mwaka 2021 katika mikoa saba.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri alisema, "USAID, tumejitolea kuwekeza na kuimarisha mifumo ya afya na kuongeza ubunifu ili kuzuia vifo vya kinamama, watoto na watoto wachanga, na vijana kwa kusaidia wanawake na watoto kupata huduma muhimu za afya zinazookoa maisha."

"Vipaumbele hivi vipo katika mkakati wetu wa ushirikiano wa kimaendeleo ambao unaweka watoto na vijana katika kiini cha mpango wetu wa miaka mitano. Kwa siku zijazo, tunafurahi kuendelea kushirikiana ili kupunguza zaidi vifo vya kinamama na watoto wachanga," alisema na kuongeza;

Somvongsiri alisema kupitia mradi mpya ambao upo kwenye mchakato wa ununuzi, wataendeleza walichojifunza kupitia mradi wa Boresha Afya na kuongeza ujuzi unaoendelea kukua na kung'aa nchini.

"Kwa siku zijazo, pia USAID itaendelea na kiwango hiki cha ushirikiano na ubia na serikali ya Tanzania na asasi za kiraia, kwani ushirikiano huu unasaidia kupata mafanikio chanya kwa watu wa Tanzania," alisema.

Taarifa hiyo ilisema kupitia ushirikiano na wa kudumu na serikali, mradi umeboresha na kuleta matokeo chanya ya afya kwa mamilioni ya Watanzania katika mikoa ya Kigoma, Simiyu, Geita, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara na Zanzibar, ikiwa ni wa miaka mitano wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 59.





CAPITAL TELEVISION

Kipindi kinachoangazia mabadiliko ya tabia nchi, Chimbuko, Madhara na njia mbalimbali za kujinasua na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na kuifanya dunia kuwa sehemu salama ya kuishi.

**USIKOSE KUFUATILIA KIPINDI HIKI KITACHOANZA SIKU YA JUMANNE TAREHE 05 OKTOBA 2021 SAA 1:30 USIKU**


# Waziri ataja dawa ujenzi holela Bahi

**Na Munir Shemweta,** BAHI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma kuongeza kasi ya upimaji ardhi katika maeneo mbalimbali ili kuepuka ujenzi holela.

Alisema, kwa sasa maeneo mengi katika halmashauri hiyo yamepanuka kimji, hivyo kunahitajika kupangwa vizuri kwa kuzingatia taratibu za mipango miji ili kuepuka ujenzi holela.

"Kwa sasa mji wa Bahi unapanuka kwa kasi na cha msingi hapa ni kuwahi kupima maeneo na kama hakuna mpango basi mji huu utakuwa na shida na cha msingi ni kuweka nguvu katika kupanga na kupima ili usiwepo ujenzi holela," alisema Mabula.

Alisema hayo wilayani Bahi wakati akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri ya wilaya hiyo akiwa katika mwendelezo wa ziara yake katika wilaya za mkoa wa Dodoma.

Katika kinachoonekana kuongeza kasi ya upimaji ardhi katika Wilaya ya Bahi, aliagiza kuundwa timu ya mkoa kwa ajili ya kupima takriban viwanja 8,000 ilivyokwama kwenye zoezi la urasimishaji makazi holela.

"Kwa kuwa kampuni zilizokuwa zikifanya urasimishaji makazi holela Bahi zimeshindwa kukamilisha kazi kwa wakati...naagiza ofisi ya ardhi mkoa kukaa na mkurugenzi wa Halmashauri ya Bahi iundwe na timu ya mkoa ije hapa kwa gharama ya mkurugenzi ili kukamilisha upimaji," alisema Dk. Mabula.

Aidha, Mabula aliitaka halmashauri hiyo kuangalia namna ya kuwawezesha watumishi wa umma kwa kuwapatia viwanja kwa makundi ili kununua kwa kulipa kwa awamu.

"Muwawezeshe watumishi wa umma kuwa na rasilimali ardhi kwa kuwaptia viwanja maana leo uko Bahi kesho uko eneo lingine na zipo halmashauri zimefanya hivyo lengo kumwezesha mtumishi kupitia sekta ya ardhi katika kumiliki na kupata makazi," alisema Mabula.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alimshukuru Mabula kwa uamuzi wa kuagiza kuundwa kwa timu ya mkoa kwa ajili ya kukamilisha upimaji wa zoezi la urasimishaji.

Aidha, aliomba halmashauri upimaji katika viwanja vyake 181 ambapo alisema kati ya viwanja hivyo ni 17 pekee ndivyo vilivyopimwa hasa ikizingatiwa eneo hilo kwa sasa linakuwa kwa kasi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Bahi eneo la Zanka ni eneo muhimu ambalo baadhi ya maeneo yake yameanza kuingia kwenye migogoro ikiwamo ile ya kuuziana mara mbili na kusisitiza eneo hilo haliwezi kuachwa bila ya kupimwa.

# Kabudi akabidhiwa Ofisi ya Mashtaka Serengeti

**Na Mwandishi wetu,** SERENGETI

SHIRIKA la Grumeti Fund linalosaidia uhifadhi na maendeleo ya jamii Serengeti, limekabidhi jengo la kisasa la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Wilaya ya Serengeti kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi.

Shirika hilo limetumia Sh. milioni 284 kujenga jengo hilo ambalo lilikabidhiwa rasmi kwa waziri huyo mjini Mugumu juzi.

Jengo hilo lenye ukubwa mita za mraba 288, lina ofisi tisa, ukumbi wa mikutano, jiko, stoo na vyoo vitatu. Katika hotuba yake ya ufunguzi wa jengo hilo, Waziri Kabudi aliishukuru Grumeti Fund kwa msaada huo, akisema ofisi hiyo itasogeza karibu na kuharakisha huduma za upelelezi na mashtaka kwa wananchi.

"Mbali ya kusogeza huduma karibu kwa wananchi, ofisi hii ya mashtaka itasaidia kukabiliana na vitendo vya ujangili mkubwa na mdogo," Prof. Kabudi alisifu.

Aliongeza: "Nimefurahi kusikia pia kuwa wadau wengine wa Grumeti Fund kama vile TAWA na TANAPA watakuwa na ofisi zao katika jengo hili jipya."

Waziri Kabudi alisema ofisi hiyo itasaidia kuipunguzia serikali gharama za kusafirisha mawakili, vielelezo na kuhudumia mashahidi.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, akizungumzia ufunguzi wa jengo hilo, alipongeza kuwa ni tukio la kihistoria kwao.

"Leo ni siku muhimu kwetu, hili ni tukio kubwa, Serengeti imekuwa wilaya ya kwanza kuwa na jengo lake la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Nitumie fursa hii kuwashukuru Grumeti Fund kwa kutujengea jengo hili," Mwakitalu alisema.

Aliongeza kuwa Wilaya ya Serengeti ina makosa mengi ya kijinai yanayohusiana na uvunjifu wa sheria za wanyamapori.

Sehemu kubwa la wilaya hiyo ni maeneo ya uhifadhi wa wanyamapori, ikiwamo Hifadhi ya Taifa Serengeti, mapori ya akiba ya Ikorongo/ Grumeti na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) ya IKONA. DPP huyo aliahidi kuongeza mawakili wa serikali na wafanyakazi wengine katika ofisi hiyo.

"Grumeti Fund itaendelea kuwa mdau na mshiriki muhimu katika mfumo wa kiikolojia wa Serengeti na ustawi wa jamii katika Wilaya za Serengeti na Bunda," Meneja Mkuu wa Grumeti Fund, Noel Mbise, alisema.

Waziri Kabudi pia aliishukuru Kampuni ya Grumeti Reserves kwa kuwekeza katika utalii unaoitangaza Tanzania kimataifa.

Alisema Grumeti Reserves imeendelea kuwa mfano wa utalii unaong'ara wilayani Serengeti.

Waziri Kabudi alilishukuru Shirika la Grumeti Fund kwa shughuli za kusaidia uhifadhi na maendeleo ya jamii.

Aliongeza kuwa mpango wa Grumeti Fund wa ufadhili wa kimasomo umewezesha mamia ya wanafunzi wa kike na kiume kutoka jamii jirani kunufaika na mpango huo.

Grumeti Fund ni shirika dada la Kampuni ya Grumeti Reserves linalojihusisha na shughuli za uhifadhi na maendeleo ya jamii katika wilaya za Serengeti na Bunda mkoani Mara.

# Asasi: Wafanyakazi wa ndani wapewe mikataba

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Sauti ya Jamii Kipunguni mkoani Dar es Salaam (CBO), Selemani Bishangazi, ameiomba serikali kuangalia kwa jicho la pili namna ya kuwawekea utaratibu waajiri wa wafanyakazi wa nyumbani kuhakikisha wanawapatia mikataba ya kazi, ili kuwatambua kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine.

Bishangazi alitoa ombi hilo katika semina iliyowakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo wafanyakazi wa nyumbani, iliyofanyika na kuandaliwa na Sauti ya Jamii jijini Dar es Salaam.

Bishangazi alisema bado wafanyakazi hao wanakutana na changamoto nyingi, ambazo baadhi yake zinatokana na kundi hilo kutokutambulika kama sehemu ya wafanyakazi.

"Bado jamii inawachukulia wafanyakazi wa nyumbani kama watu wa chini na wasio na thamani yoyote na ndiyo maana,

wamekuwa wakikutana na changamoto nyingi, ambazo na wao kutokana na namna jamii inavyowachukulia, wanakosa ujasiri wa kulalamika popote," alisema Bishangazi.

"Wapo baadhi, ambao wakati mwingine hawalipwi kabisa stahiki zao na waajiri wao na ndiyo maana tunaiomba serikali iliangalie hili kwa jicho la pili, angalau kuwe na utaratibu wa waajiri kuwapa mikataba, ili wanaponyimwa haki zao wadai kisheria."

Bishangazi alisema wamekuwa wakikumbana na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi hao kufukuzwa kazi pasipo kupewa stahiki zao.

"Tunapokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi hawa, wengi wanakimbilia ofisini kwetu wanapokuwa wamefukuzwa kazi na ukifuatilia wengi wao wanafanyiwa hivyo baada ya kushindwana na waajiri wao na miongoni mwa sababu ni kutakwa kimapenzi," alisema Bishangazi.

"Kwa hiyo binti anapomkataa bosi wake kuwa naye kwenye mahusiano ya kimapenzi, anamfukuza kama mbwa, bila hata ya kumpatia mshahara wake na wakati mwingine unakuwa umelimbikizwa hata zaidi ya miezi mitatu au mitano na ndiyo maana tunasema endapo wangekuwa na mikataba ya kazi ni rahisi kudai kwenye vyombo vya sheria."

Agness Riziki alisema yeye alifukuzwa kazi na mwajiri wake baada ya kutakwa kimapenzi na hakupewa malipo yake ya miezi mitatu.

"Nilikuwa nimefanya kazi kwa miezi saba tu, miezi minne ya mwanzo nililipwa vizuri, lakini nilipofikisha mwezi wa tano nikaambiwa nisubiri hawajapata pesa ya kunilipa na wakati huo bosi wangu alikuwa ameanza kunitaka kimapenzi, lakini nikawa sijakubaliana naye, hali hiyo iliendelea nikafikisha miezi minne bila kulipwa, bosi wangu aliniambia hawezi kunilipa mpaka nimkubali na nilipoendelea kubishana naye alinifukuza kazi na hakunilipa tena," alisema Agness.

# Korosho zote kupitia Bandari ya Mtwara

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema Bandari ya Mtwara itatumika kusafirisha korosho na uamuzi huo hautabadilika, kwa kuwa ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Vilevile, amepiga marufuku matumizi ya kangomba kwenye mauzo ya zao hilo, akisisitiza utaratibu huo utachelewesha kuuzwa kwa bei nzuri na watu kuandaa mashamba kwa wakati.

Aliyasema hayo mjini Mtwara, juzi alipotembelea bandari hiyo, kwa lengo la kuangalia kama maelekezo ya Rais kuhusu korosho yote kusafirishwa kupitia bandari hiyo, yametekelezwa.

"Haya ni maelekezo ya serikali kwamba korosho yote huku, itapitia bandari hii, maagizo hayo ni ya Rais, hayatabadilika. Kwa hiyo, wote ambao wanataka kufanya biashara ya korosho wajipange.

"Zaidi ya hapo hapa bandarini wanafanya kazi saa 24, kwa hiyo meli ikija kama ni kupakia inapakia kwa muda na kasi sana, kwa sababu ya uwezo huo wa kufanya kazi muda wote," alisifu.

Waziri huyo alisema serikali imeshatoa kibali wanaosafirisha korosho kuleta Bandari ya Mtwara wanaruhusiwa kufanya hivyo kwa saa 24, hivyo wameshatengua kanuni zilizokuwa zinaelekeza baada ya saa 12, huwezi kusafirisha zao hilo.

Alisisitiza kuwa mtu akitaka kununua korosho, lazima apitishe kwenye bandari hiyo kwa kuwa gharama zimepunguzwa, hivyo kuokoa fedha nyingi, ambazo zingetumika kusafirisha kwa njia nyingine.

"Tunasisitiza si kwa sababu tunataka bandari hii ifanye kazi, bali uzoefu unaonyesha, kwamba korosho inaponunuliwa kutoka Mtwara, yenye ubora inaposafirishwa mpaka Dar es Salaam baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa wakiiharibu kwa kuongeza vitu au kuweka isiyofaa," alisema.

Katika hatua nyingine, waziri huyo amepiga marufuku matumizi ya kangomba, kwa kuwa utaratibu huo utachelewesha kuuza kwa bei nzuri bidhaa hiyo na watu kuandaa mashamba kwa wakati.

Naibu Waziri wa kilimo, Hussein Bashe, alisema wataendelea kufanya kazi na Mamlaka ya Bandari na kupitia kikao kitakachofanyika Alhamisi, jijini Dar es Salaam, watajadili hoja mbalimbali zilizotolewa na wasafirishaji wa zao hilo.

Alizitaja baadhi ya hoja hizo ni gharama ya uhifadhi, upatikanaji wa makasha, muda wa kuhifadhi makasha ya wasafirishaji, ambao kwa sasa umeongezwa kutoka siku 14 mpaka 21, uwezo uliopo ni kuhifadhi makasha 13000 kwa wakati mmoja, hivyo hakuna tatizo.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Karim Mattaka, alisema wapo tayari kuhudumia shehena hiyo, kwa kuwa wameongeza uwezo wa kuhifadhi na kuhudumia korosho kwa kuongeza eneo na vifaa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na viongozi wa Serengeti Breweries (SBL), kwenye maadhimisho ya uwekezaji wa miaka mitatu wa kampuni hiyo, katika kiwanda cha SBL, mkoani Kilimanjaro jana. Kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni hiyo, John Ulanga na Mkurugenzi wa Operesheni, Anthony Njenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SBL sasa yawekeza bil. 166/- kujipanua

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imeadhimisha safari yake ya uwekezaji wa miaka mitatu inayogharimu Sh. bilioni 166 inayolenga kuongeza uwezo wake wa uzalishaji pamoja na kuzindua kiwanda kipya cha kutengeneza pombe kali.

Mpango huu ulianzishwa mwaka 2019 ambapo SBL ililenga kuongeza uzalishaji wake katika viwanda vyake vilivyopo Dar es Salaam, Mwanza na Moshi. SBL pia imezindua kiwanda kipya na cha kisasa cha kutengeneza pombe kali mjini Moshi ikiwa sehemu ya mpango wake wa uwekezaji.

Akizingumza mbele ya mgeni rasmi wa shughuli hiyo ambae alikuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema: "Upanuzi huu utasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya nafaka za ndani ambazo SBL inanunua kwa wakulima nchini kama mahindi, shayiri na mtama kwa ajili ya kutengeneza bia.

Vilevile, itatengeneza fursa za ajira na kupanua uwezo wa kampuni kusambaza bidhaa zake nchini. Aidha, upanuzi huu umekusudia kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi ya Serikali na hivyo kuiongezea nchi mapato."

Ocitti alisema kiwanda hicho kipya kitatengeneza pombe kali za ndani katika viwango vya kimataifa na kuiwezesha SBL kuwa mshindani mkubwa katika uzalishaji wa pombe kali, na kwamba kabla ya uanzishwaji wa kiwanda hicho, SBL ilikuwa inaagiza pombe kali kutoka nje.

Waziri Mkuu alipongeza SBL kwa kuwekeza zaidi nchini, jambo ambalo litaisadia nchi kupata mapato zaidi na kuchochea ukuaji wa kiuchumi. Majaliwa alisisitiza dhamira njema ya Serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Kiwanda kipya cha kutengeneza pombe kali mjini Moshi kimejengwa kwa gharama za shilingi bilioni 15.6. Gharama hizi ni miongoni mwa safari ya uwekezaji wa miaka mitatu ambapo SBL imepanga kutumia bilioni 124 kuongeza uzalishaji wake wa pombe, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa SBL.

Kiwanda hicho kipya kitatengeneza aina mbalimbali za pombe kali hadi zile zilizokuwa zinaingizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, SBL ilishaanza kutengeneza pombe kali mpya nchini iitwayo, BONGO DON ambayo Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa utengenezaji wake umezingatia viwango vya kimataifa.

SBL imeajiri wafanyakazi 800 na maelfu wengine wakifaidika katika mnyororo wake wa thamani. SBL ina mtandao wa wakulima zaidi ya 400 nchini ambao wanautumia kununua nafaka za kuzalisha bia kama mahindi, shayiri na mtama.

**HABARI KITAIFA**

# Chalinze sasa kuanza kupata maji wakati wote

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WAKAZI wa Chalinze Wilaya ya Bagamoyo mkoa wa Pwani wanatarajia kuondokana na kero ya maji inayowakabili kwa muda mrefu ifikapo mwezi ujao utakapokamilika mradi wa maji Mlandizi-Mboga.

Hayo yalielezwa jana na Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) Mkoa wa huduma wa Chalinze, Mhandisi Paschal Fumbuka, wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kusikiliza kero za wananchi na kukagua miradi.

Mhandisi Fumbuka alisema kukamilika kwa mradi huo kutaondoa kero ya kukatika kwa maji mara kwa mara, ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wakazi wa mji wa Chalinze na maeneo ya jirani.

Meneja huyo alisema uwezo wa mitambo iliyopo sasa ni kuzalisha maji mita za ujazo 7,500 huku mahitaji yakiwa 15,000.

Aidha, alieleza kuwa mradi wa Mlandizi-Mboga utakapokamilika kwa siku utakuwa na uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 9,000 na kuondoa kero iliyokuwapo awali.

Mhandisi Fumbuka alisema hakuna mfanyakazi anayehujumu usambazaji wa maji kwa manufaa binafsi, hivyo aliahidi kuzingatia maelekezo ya Mkuu wa Mkoa ya kuhakikisha wateja wa majumbani wanapata maji kama ilivyo katika maeneo mengine.

Akikagua mradi huo, Kunenge alitoa maelekezo kwa mamlaka hiyo kuhakikisha mradi huo utakapoanza kazi maji yafike kwa wananchi muda wote.

Baadhi ya wakazi wa Chalinze walimweleza Kunenge kuwa kuna kero ya upatikanaji wa maji ambapo wakati mwingine wanakaa wiki mbili hadi tatu bila huduma hiyo.




Mratibu wa uwekezaji Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Gaudence Nyamwihura (katikati), akijaribu ubora wa moja ya matrekta yatakayotolewa kwa washindi wa kampeni ya 'Vuna zaidi na NBC Shambani' mahsusi kwa wakulima wa korosho mikoa ya Lindi na Mtwara, wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, mjini Lindi mapema wiki hii. Kulia ni Mkuu wa Bidhaa na Mauzo wa benki ya NBC, Abel Kaseko na Meneja wa Benki hiyo, mkoa wa Lindi, Iovin Mapunda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni yawavuta wakulima wa korosho

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

CHANGAMOTO ya huduma za kifedha iliyokuwa ikiwakabili wakulima wa korosho mikoa ya Mtwara na Lindi ikiwamo kutopata mikopo kwa wakati na makato ya fedha zao wanapofanya miamala ya kibenki, imetajwa kuwa miongoni mwa sababu kubwa za kuvutiwa zaidi na kampeni ya kuwahamasisha kuongeza uzalishaji.

Kampeni hiyo ambayo wanaeleza kuwa imewahamasisha ni ya 'Vuna zaidi na NBC Shambani' inayoendeshwa na benki ya NBC mahususi kwa mikoa hiyo.

Wakizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo mkoani Lindi jana na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa zao hilo wakiwamo viongozi wa kiserikali, viongozi vyama vya msingi (AMCOS) na vyama vikuu vya ushirika, wakulima hao walisema ujio wa kampeni hiyo umewahamasisha zaidi kujiunga na huduma ya NBC Shambani ili kujikwamua kutoka kwenye changamoto hizo zilizotajwa kukwamisha jitihada zao za kujikwamua na umaskini kupitia kilimo cha zao hilo.

"Pamoja na uwapo wa zawadi mbalimbali kwenye kampeni hii kama baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa, maguta pamoja na matrekta zaidi pia tumevutiwa sana akaunti husika kwa kuwa inajibu changamoto kadhaa zinazotukabili kwenye huduma za kifedha ikiwamo ucheleweshwaji wa mikopo na makato yaliyokithiri," alisema Swalehe Juma, Mwenyekiti wa Nachunyu AMCOS mkoani Lindi.

Walisema changamoto ya ucheleweshwaji wa mikopo imekuwa ikisababisha wengi wao kupata fedha wakati usio sahihi kulingana na mahitaji yao ya kilimo, hivyo kujikuta wakitumia mikopo hiyo kwa shughuli zisizoendana na kilimo.

"Tunashukuru kuona kwamba NBC wameamua kubuni huduma mahusus kwa ajili yetu... tukiwa kama viongozi wa vyama vya msingi tumeipokea vema huduma hii na tumejipanga kuhakikisha kwamba inawafikia wanachama wetu wote kwenye maeneo yetu," aliongeza.

Mkuu wa kitengo cha wateja wadogo wadogo na wakulima kutoka Benki ya NBC, Raymond Urassa, alisema licha ya uwapo wa huduma ya NBC Shambani kwa zaidi ya mwaka sasa benki hiyo imebuni kampeni hiyo ili kuhakikisha kila mkulima wa korosho anafikiwa na huduma hiyo ili kwa pamoja waweze kufikia adhma ya kuleta mapinduzi ya kilimo kupitia zao hilo.

"Nii kampeni inayolenga kuhamasisha mapinduzi ya kilimo cha korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara na ndio sababu hata zawadi zinazotolewa kupitia kampeni hii ikiwemo pikipiki, pampu za kupulizia dawa na matrekta zinalenga kumsaidia mkulima aweze kustawisha kilimo chake," alifafanua.

Akizungumza wakati akifungua kampeni hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mratibu wa uwekezaji Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, Gaudence Nyamwihura, pamoja na kuwasisitiza wakulima hao na AMCOS kuchangamkia kampeni hiyo, pia aliwasisitiza kubainisha vipaumbele vyao wanapoamua kukopa kwenye taasisi za kifedha ili matumizi ya mikopo hiyo iwe na tija zaidi kwao.

Uzinduzi wa kampeni hiyo ulienda sambamba na uzinduzi wa huduma ya bima ya afya kwa wakulima wa zao hilo inayotolewa na benki hiyo kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) pamoja utoaji wa msaada wa pikipiki na baiskeli zilizotolewa na benki hiyo kwa AMCOS za mkoa huo kwa ajili ya kurahisisha shughuli za kiutendaji.

## Wazazi kuadhibiwa utoro watoto shuleni

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema kuanzia sasa mwanafunzi atakayebainika kuwa mtoro adhabu itatolewa kwa mzazi na mtoto.

Kunenge alitoa agizo hilo jana alipokuwa katika ziara ya kusikiliza kero za wananchi na kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wikaya ya Chalinze.

Akiweka jiwe la msingi ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu Shule ya Sekondari Vigwaza, alisema wazazi wanatakiwa kufuatilia mwenendo wa watoto wao badala ya kuacha kazi hiyo kwa walimu.Kunenge alisema mwanafunzi yeyote atakayebainika kuwa mtoro, adhabu itatolewa kwa wanafunzi na wazazi kukomesha hali hiyo.

Aidha, akiwa katika ziara hiyo ya kata kwa kata alimuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze kuangalia uwezekano wa kumaliza uhaba wa matundu ya vyoo katika shule hiyo ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kwa wanafunzi.

## Kampuni ya madini yafagilia maonyesho

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya OreCorp Tanzania Ltd imeeleza kufurahishwa kushiriki na kuunga mkono maonyesho ya teknolojia ya uchimbaji madini na uwekezaji yanayoendelea katika viwanja vya Bombambili mkoani Geita.

Maonyesho hayo yaliyofunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, yanatoa nafasi kwa wadau kuungana na kuchangia mawazo na ujuzi wa namna ya kukuza teknolojia ambayo itasaidia kuchochea maendeleo ya sekta ya madini nchini.

Akizungumza wakati wa maonyesho hayo, Meneja Mkuu wa OreCorp, Damien Valente, alisema kwa mara nyingine maonyesho hayo yamekuwa na mafanikio makubwa na OreCorp inajivunia kuwa sehemu yake mkoa wa Geita na maendeleo endelevu ya taifa ambalo linaongoza katika uzalishaji wa dhahabu.

OreCorp imesema mipango yake ya baadaye ni kuendeleza ujenzi wa mradi wa dhahabu wa Nyanzaga.

Alisema maonyesho yamefanyika katika wakati muhimu kwa OreCorp ambayo Juni 02, 2021 ilipata idhini kutoka Baraza la Mawaziri wa Tanzania lilipoidhinisha maombi ya leseni maalum ya uchimbaji madini kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa mgodi wa dhahabu wenye thamani ya Sh. bilioni 670 kusini mwa Kata ya Ngoma katika Wilaya ya Sengerema.

Alisema mradi huo upo mbioni kuwa mgodi mkubwa zaidi wa dhahabu kuwahi kujengwa Tanzania kwa zaidi ya muongo mmoja na wa kwanza kuwahi kujengwa ndani ya Wilaya ya Sengerema.

Mradi wa dhahabu wa Nyanzaga upo wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza na unakadiriwa kuwa na wakia milioni tatu za dhahabu na utazalisha kiasi cha wakia 200,000 (tani sita) za dhahabu kwa mwaka na ujenzi wake utagharimu shilingi za kitanzania bilioni 670.




Kwaheri Profesa Matthew Laban Pimpa Luhanga




# BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 24, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Karibu Januari, uwe na uchungu

UBIA WA TARI, JKT, MAGEREZA...

# Mradi wa kipekee kutumia michikichi Kigoma kumaliza uhaba mafuta ya kula

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

MAHITAJI ya mafuta ya kula nchini ni makubwa, lakini uzalishaji wake ni mdogo. Sababu ni malighafi yake kama alizeti, ufuta, michikichi, nazi na pamba yanalimwa kwa kiwango kidogo.

Wakati uzalishaji wa mafuta ya kula nchini ni tani 205,000, mahitaji yanagota katika tani 570,000, ikiwa nakisi ya upungufu tani 365,000.

Mwaka 2019, serikali iIibuni mkakati wa kupanua kilimo cha michikichi, ikianzia na mkoa Kigoma na baadae kusambaa kwingineko inakositawi, kupatikana mafuta mawese kwa wingi, ikiaminika inatoa mafuta mengi, ikilinganishwa na alizeti, ufuta, pamba, karanga na soya.

Hata hivyo, mchikichi unalalalamikiwa kulimwa kienyeji kwa miaka mingi, hasa mkoani Kigoma, hata wananchi kutoona umuhimu wake.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Mkuu Majaliwa Kassim, aliiagiza Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI) kufufua michikichi Kigoma, ikianza na utafiti wa mbegu bora.

TARI ilitafiti na kuibua mbegu bora na ya kisasa inayoitwa Tenera, ikitokana na zao mchanganyiko wa mbegu ya dura na pesifera, ambazo zimekuwa zikitumika muda mrefu na wakulima hao.

Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha TARI, Kihinga mkoani Kigoma, Dk. Filson Kagimbo, anasema utafiti huo wamebaini mbegu ya Tenera, ina uwezo wa kutoa wastani wa tani tano mpaka sita ya mafuta ya kula kwa hekta moja.



Kamanda wa Magereza Mkoa wa Kigoma na Mkuu wa Gereza la Kwitanga, Bosco Mgema (katikati), akimwonyesha Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, mti wa mchikichi aina ya Tenera ulioanza kuzaa, baada ya kupandwa na Waziri Mkuu Kasim Majaliwa mwaka 2019, alipozindua mbegu bora, gerezani hapo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

Dk. Kagimbo anasema wameshafanikiwa kugawa bure mbegu hizo kwa halmashauri nane za mkoa Kigoma na taasisi za kijeshi, ikiwamo Gereza la Kwitanga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kikosi 821 Bulombora.

Anasema, TARI imeshazalisha miche bora ya kisasa ya michikichi Tenera milioni 6,850,166 kwa ufadhili wa serikali, kutekeleza mpango uliopo serikalini.

Dk. Kagimbo anasema miche ya michikichi inayotoa mafuta wastani wa tani tano mpaka sita kwa hekta, imezalishwa kwa kuunganisha kati ya mche wa zamani aina dura.

Anasema, miche hiyo ya kisasa aina ya tenera imewezeshwa kuzalishwa kutokana na ufadhili wa serikali, kwani ni miche inayouzwa na asasi binafsi kwa bei wastani wa Sh.10, 000.

Dk. Kagimbo anazitaja halmashauri zilizogaiwa miche hiyo bure, ni Kasulu, Kigoma, Kasulu Mji,Uvinza ,Kigoma Manispaa na Buhigwe, hatua iliyoendana na kutoa elimu kwa maofisa ugani wa kata zote wawasaidie kutoa ushauri wa kilimo hicho.

Mtaalamu huyo, pia Mratibu Kitaifa wa zao Michikichi, anasema nchini mafuta yanayotumika kwa mlo ni asilimia 60 hadi 64, huku mafuta mchikichi huo unaoliwa takriban asilimia 99.3 unaagizwa kutoka nje ya nchi.

### MAFANIKIO YALIVYO

Jitihada za utafiti huo wa mbegu bora ya mchikichi kupitia utafiti na TARI umeanza kuonyesha matokeo chanya baada ya uzinduzi kupitia mche wa mbegu uliopandwa na Waziri Mkuu Majaliwa, Kassim Majaliwa, mkoani Kigoma.

Mche wa Mchikichi uliopandwa na Waziri Mkuu Majaliwa mwaka 2019 katika uzinduzi wa upandaji mbegu bora ya mchikichi katika kitalu cha Gereza la Kwitanga, mkoani Kigoma sasa umeshaanza kutoa matunda, ikiwa ishara ya kuanza kuzaa michikichi katika kipindi cha miaka miwili tu.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, anasema matokeo hayo ya mbegu ya Tenera yamepatikana kabla ya muda miaka mitatu uliokadiriwa kuanza uzalishaji.

“Waziri Mkuu alikuja kuzindua mche bora wa kisasa aina ya Tenera mwaka 2019 na katika utafiti uliofanywa ulipaswa kuanza uzalishaji katika kipindi cha miaka mitatu tangu kupandwa, lakini ndani ya miaka miwili tayari umeshazaa haya,” anasema.

Dk. Mkamilo anasema mbegu hiyo ya kisasa aina ya Tenera serikali imezigawa bure kwa walima mchikichi wa Kigoma, ili kuliendeleza zao hilo kwa wazalishaji mafuta ya kula, ikiwa hatua iiliyowasaidia wakulima kuhama kutoka mbegu za miaka saba hadi miwili.

“Mbegu ya Tenera inatoa wastani wa tani tano mpaka sita za mafuta ya kula kwa hekta moja na ile ya zamani aina ya Dula inayotumiwa na wakulima wengi inatoa tani 1.5 kwa hekta,” anafafanua Dk, Mkamilo.

Mkurugenzi huyo wa TARI, anasema Wizara ya Kilimo inaweka mikakati ya kuhakikisha inamaliza tatizo la uhaba wa mafuta ya kula nchini.

Pia, anasema kuwa ni mpango utakaoisaidia serikali kuokoa

INAENDELEA UK.14

MAKALA MAALUM

# Kwaheri Profesa Matthew Laban Pimpa Luhanga

**Na Mark Mwandosya**

NIMEOMBWA na familia ya Matthew Laban Pimpa Thompson Alfred Luhanga niongee machache kwa niaba yao kama njia ya kutoa shukrani kwa kadamnasi hii na wote mliohusika kwa njia mbalimbali kuifariji familia katika kipindi hiki kigumu.

Ni kweli nimeombwa, lakini nami pia nilitaka iwe hivyo, ili nitumie nafasi hii, ukumbi huu, mahala hapa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, niweze kumuaga ndugu na rafiki wa karibu, profesa mwenzangu wa teknolojia ya umeme, elektroniki na mawasiliano, mwanafunzi mwenzangu, mhandisi mwenzangu, mwandishi mwenzangu na jirani yangu.

Nafanya hivyo, pia kwa niaba ya familia yangu, mke wangu Lucy, vijana wetu: Max, Sekela na Emmanuel, na ukoo wote wa Mwandosya na wa Magombe, walio hai na waliotutangulia mbele ya haki.

Nimezoea kutoa mihadhara kama mwalimu hapa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vikuu vingine. Kama mtumishi wa umma, nimehutubia mikutano mbalimbali na maeneo mbalimbali nchini na duniani kote.



Profesa Mark Mwandosya, aliposhiriki kumuaga, Marehemu Profesa Mathew Luhanga.

Nakiri kwamba hakuna uzoefu unaokutayarisha kutoa salaam za kuomboleza na kutoa shukrani, hasa pale ambapo anayekutoka alikuwa mtu wa karibu sana.

Nitajitahidi na nikiazima maneno ya Mark Anthony alipotoa salaam zake katika maziko ya Juliasi Kaisari, "Wanazuoni, ndugu zangu, naomba masikio yenu", nikimaanisha, "naomba mnisikilize, mnivumilie".

Aliyesoma wasifu wa Matthew amefanya kazi nzuri sana na kwa umahiri mkubwa. Amenirahisishia kazi yangu. Amejibu swali kuu linaloulizwa na litaendelea kuulizwa, "Profesa Matthew Luhanga alikuwa nani hasa?"

Lakini wengi pia wameniuliza, "Profesa Mwandosya, ukaribu wako na Profesa Luhanga umeanzia wapi?" Maelezo yangu yatakuwa mafupi na yatajikita katika yale mambo ambayo hayaandikwi katika wasifu, lakini ambayo kwangu yametufanya mimi na yeye na familia zetu kuwa karibu.

Ni mchanganyiko wa bahati, hatima na matukio ambayo sio rahisi kujua chanzo chake. Wakati mwingine nadiriki kusema yanatokana na sababu za kiroho zaidi.

Niliingia darasa la tisa (kidato cha kwanza) Shule ya Sekondari ya Serikali Malangali Januari mwaka 1965, wakati ule sisi wanafunzi wa kidato cha kwanza tukiitwa 'Mugya'. Hapo nilimkuta Matthew akiwa darasa la 10 (kidato cha pili). Hawa vijana wa kidato cha pili walituendesha vilivyo, mithili ya magaidi.

> "Suala la mabadiliko ya tabianchi sasa linazungumzwa sana duniani. Matthew na mimi tulilifanyia utafiti miaka 25 iliyopita.

Hata hivyo, Matthew alikuwa mstaarabu katika kundi hilo. Tukajenga urafiki kwa sababu mbili. Mosi, wote tulikuwa tunatoka Mbeya Mjini na pili tulikuwa na uwezo mkubwa wa masomo yote, ikiwa ni pamoja na hisabati.

Kuhusu hisabati, mimi na yeye tulikuwa tunawasaidia wanafunzi wa kidato cha tatu katika somo la hilo, ikiwa ni pamoja na somo la hisabati ziada (Additional Mathematics).

Mwaka juzi, Mwalimu Ambangile Mwakilembe, Mwalimu Charles Muhitira, na Mwalimu Clement Bendera walikuja kunitembelea kijijini, Lufilyo, Busokelo, kuhudhuria kumbukumbu ya miaka 70 ya kuzaliwa kwangu.

Mwalimu Mwakilembe akatukumbusha jinsi Matthew na mimi tulivyoweza kugundua makosa katika kitabu maarufu cha hisabati cha Durell, jambo ambalo lilichangia masahihisho yafanywe katika makala zilizofuata.

Nakumbuka siku moja, Matthew akiwa kidato cha nne na mimi cha tatu, Mwalimu Mkuu, Alexander Thobias Mabele, marehemu baba ya mwenzetu Profesa Robert Mabele (ambaye naye ni marehemu. Mwenyezi Mungu awarehemu), aliitisha mkutano wa wanafunzi na walimu.

Akasema alikuwa na neno moja tu, nalo ni kwamba Malangali ilikuwa na bahati ya kuwa na wanafunzi wawili wenye vipaji vya hali ya juu. Kila mtu akatega masikio Mwalimu Mabele atasema nini. "Na wanafunzi hao ni Matthew Luhanga na Mark Mwandosya". Akafunga mkutano, akaondoka, akituacha na butwaa. Lakini, mimi nilihisi alimlenga zaidi Matthew.

Alipomaliza kidato cha nne, Matthew akachaguliwa kwenda Chuo cha Ufundi cha Dar es Salaam (DarTech) ili yeye na wenzake waanzishe kidato cha tano, mchepuo wa Hisabati, Hisabati, Fizikia (Pure Mathematics, Applied Mathematics, Physics-PMM), mchepuo ambao ulilenga katika kutayarisha vijana kwenda vyuo vikuu kusomea uhandisi. Nilimkuta Matthew DarTech mwaka 1969 nilipochaguliwa kuingia hapo kuchukua mchepuo huo wa PMM. Alipomaliza kidato cha sita, Matthew alijiunga na Chuo Kikuu cha California Polytechnic (California State Polytechnic University, Pomona, California) kusomea shahada ya kwanza ya uhandisi umeme na elektroniki na akufuzu kwa kiwango cha juu (suma cum laude).

Akaendelea hapo hapo na kupata shahada ya uzamili. Nami nilipohitimu kidato cha sita, nikapata udhamini wa kwenda kusomea uhandisi umeme Chuo Kikuu cha Aston, Uingereza.

Nilipofuzu na kupata shahada ya kwanza daraja la kwanza (first class honours), nikaenda Chuo Kikuu cha Birmingham moja kwa moja kufanya utafiti na kuhitimu shahada ya uzamivu katika fani ya umeme na teknolojia ya elektroniki, baada ya miaka miwili na nusu.

Aliporudi kutoka Marekani, Matthew akawa mkufunzi Dar Tech, kama sharti la ufadhili wake kwenda Marekani lilivyomtaka. Nami nilipomaliza masomo yangu nikaja kuwa Mhadhiri, Idara ya Umeme, Kitivo cha Uhandisi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Akiwa Dar Tech na mimi nikiwa UDSM, mimi na Lucy tulipofunga ndoa, Matthew na mkewe Stephania (sasa ni marehemu na apumzike kwa amani) ndio waliosimamia ndoa yetu.

Enzi hizo hatukuwa gari. Tulipanda magari ya Usafiri Dar es Salaam (UDA) kwenda kufunga ndoa. Baada ya hapo apo tukachukua UDA tena kwenda kwa kina Matthew na Stephania hapo DarTech kwa ajili ya chakula cha mchana.

Baadaye sisi tukarudi Barabara ya Kileleni, Nyumba Namba 25, Chuo Kikuu cha Dar es Saam. Gharama za harusi hazikuzidi shilingi mia tano.

Ilikuwaje Matthew akaja kuwa Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam? Kuna wakati nilikaimu kama Mkuu wa Idara ya Umeme, Kitivo cha Uhandisi hapa UDSM. Moja ya majukumu nyangu ilikuwa ni kutafuta na kuwashawishi Watanzania wenye uwezo wajiunge na Idara kama wahadhiri.

Nilipomshauri Matthew ajiunge nasi na alipokubali, ndipo nilipomuendea Profesa Awadhi Sadiki Mawenya, aliyekuwa Mtanzania wa kwanza kuwa Mkuu wa Kitivo Cha Uhandisi, kumwomba akubali tuanze mchakato wa kumhamsha Matthew kutoka DarTech kuja UDSM.

Profesa Mawenya akakubali kuchukua jukumu hilo na akaomba ridhaa ya ndugu Ibrahim Kaduma, aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Naye akakubali. Wizara ya Elimu walionyesha ugumu kumruhusu ahamie Chuo Kikuu.

Nikachukua jukumu la kumwona aliyekuwa Waziri wa Elimu, nadhani alikuwa Mheshimiwa Nicholas Kuhanga. Waziri akamuagiza Katibu Mkuu atoe kibali husika mara moja. Na kama wahenga walivyosema, yaliyofuata sasa ni historia.

Baada ya Malangali na DarTech kama wanafunzi, tukaja kukutana Uhandisi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama wahadhiri.

Tukakutana tena Marekani mwaka 1983, yeye akiwa Chuo Kikuu cha Columbia, New York, akisomea shahada ya uzamivu na mimi nikiwa likizo ya sabato (sabathical leave), Chuo Kikuu cha Princeton, New Jersey.

Tuliporudi kutoka Marekani, baada ya muda mfupi mimi nikateuliwa kuwa Kamishna wa Nishati na Petroli, baadaye Katibu Mkuu, halafu Waziri katika Wizara mbalimbali na hatimaye Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, kama mwanzilishi.

Yeye akaendelea na utumishi wa chuo kikuu na akateuliwa kuwa Ofisa Mkuu Taaluma na baadaye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tukiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hata baada ya mimi kuazimwa na hatimaye kuhamia serikalini, kwa pamoja tumetoa maandiko kadhaa yaliyochapishwa katika majarida ya kutaaluma humu nchini na nje ya nchi.

Nilikuwa napitia wasifu wake nikaona ana machapisho zaidi ya 75 na vitabu nane. Vinne kati ya hivyo nane tumeandika pamoja katika fani za uhandisi, nishati na mazingira, hususan mabadiliko ya tabianchi.

Suala la mabadiliko ya tabianchi sasa linazungumzwa sana duniani. Matthew na mimi tulilifanyia utafiti miaka 25 iliyopita.

Matthew na mimi tulianza uandishi wa pamoja zamani kidogo, tukiwa wanafunzi wa sekondari. Mwaka 1970 tuliandika makala kuhusu umuhimu wa Tanzania kuwa na wahandisi wanawake. Makala hiyo ilichapishwa katika gazeti la kila siku la serikali, The Standard, Tanzania, toleo Namba 12, 344, chini ya kichwa, 'Why No Women Engineers?' Makala hiyo, iliyotoka tarehe 10 Julai 1970 na ikawa ni makala bora ya wiki, na tukapata zawadi ya shilingi 20.

Chapisho letu la pamoja la mwisho limetoka miezi michache tu iliyopita. Yeye na mimi tukiwa waandishi wenza, tumechapisha andiko kuhusu, "Blockchain: A Disruptive and Transformative Technology of the Fourth Industrial Revolution", andiko ambalo limo katika jarida la kitaaluma la Shule ya Biashara, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam Business Management Review).

Profesa Luhanga ndiye aliyeishauri Idara ya Umeme, Kitivo cha Uhandisi ianzishe Kigoda cha Uprofesa/Kiprofesa cha Usimamizi wa Nishati na Teknolojia (Professorial Research Chair in Energy Technology and Management), Kigoda cha kwanza kuanzishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kigoda ambacho nilibahatika kuwa profesa wa kwanza kukikalia.

Kilipoanzishwa kigoda cha teknolojia na usimamizi wa mawasiliano, Profesa Luhanga akawa profesa wa kwanza kigoda hicho.

Profesa Luhanga ndiye aliyewezesha kupatikana kwa eneo linalotumika na Chuo cha Teknolojia za Habari na Mawasiliano cha UDSM, kilicho pale Kijitonyama, baada ya Mark Mwandosya, aliyekuwa Waziri mwenye dhamana ya sekta ya mawasiliano, kumshauri aiombe serikali, ili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kipewe eneo hilo, majengo yaliyokuwepo na miundombinu yake.

Lakini, Profesa Luhanga atakumbukwa zaidi kwa kubuni na kutekeleza kimkakati na kwa ufanisi mkubwa, Programu wa Mageuzi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam Institutional Transformation Programme). Programu hiyo iliongeza ufanisi katika utendaji kazi, ilipanua wigo na kuongeza udahili wa wanafunzi.

Pia, ilileta matumizi bora ya majengo na kuongeza miundombinu; na ilifanikiwa kuleta uwiano mzuri wa kijinsia katika udahili. Wote tumeshuhudia matokeo chanya ya mabadiliko hayo.

Moja ya mambo ambayo hayajulikani sana ni kwamba Profesa Luhanga, Profesa Mawenya, Ndugu Enock Kamuzora, Mhandisi Ladislaus Salema, Ndugu Ibrahim Kaduma na sisi wengine, tulikuwa waanzilishi wa kikundi cha kubuni mbinu na mikakati ya kuzuia rushwa katika sekta ya uhandisi na hasa katika ujenzi (FACEIT-Front Against Corruption in Engineering in Tanzania). Hii ilikuwa hata kabka ya Tume ya Warioba.

Mambo mengine yalikuwa si rahisi kuyaelewa yalivyotokea. Baruany Elijah Luhanga, kaka yake Matthew, ambaye alituchemsha sana tukiwa 'mugya' Malangali, ndiye aliyenikaribisha Uingereza akiwa mwanafunzi wa uhandisi wa elektroniki Chuo Kikuu cha Liverpool, Uingereza, mimi nilipokwenda Aston.

Tukaja kukutana tena yeye akiwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, mimi nikiwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, wizara iliyokuwa na jukumu la kuisimamia TANESCO.



Aliyekuwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia Prof. Peter Msolla, akimtunuku cheti cha mshindi wa kwanza Prof. Matthew Luhanga wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam kufuatia Taasisi ya Kompyuta ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kushika nafasi ya kwanza wakati wa sherehe ya kutoa tuzo za taifa za ugunduzi na ubunifu na kutoa Mwega kwa ajili ya utafiti mwaka 2010, jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA MAALUM**

Jambo ambalo lilistaajabisha familia zetu ni pale mama yao akina Luhanga, Mama Edith Talina Nyamkandawire, na baba yetu sisi, Mzee Isaac Mwandosya, walipofariki siku moja hapa Dar es Salaam mwaka 1995. Tukawa na misiba miwili na misafara miwili ya kwenda kuzika huko Mbeya.

Nilipokuwa nafundisha Control Theory EE441 hapa Chuo Kikuu, kipindi hicho kilikuwa cha dakika 50. Ikifika dakika 40 baadhi ya wanafunzi walikuwa wanaanza kupiga miayo. Nikiwauliza, "Kwanini?" Wanasema, "Njaa Profesa". Nisingependa baadhi yenu muanze kupiga miayo.

Hivyo basi, nimalizie kama nilivyoanza na kama nilivyoombwa, kwa kuwashukuru wote mliyokuja kumsindikiza ndugu yetu Profesa Matthew Luhanga, au Uncle Matthew, kama watoto wetu wanavyomfahamu. Tunawashukuru madaktari, wauguzi na wengine waliomhudumia Uncle Matthew hapa nchini na huko India.

Tunatambua na kuheshimu uwepo kati yetu wa uwakilishi kutoka serikalini. Tunamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ambaye amewakilishwa na Profesa Kitila Mkumbo, profesa mwenzetu na Waziri wa Viwanda na Biashara. Uwapo wa Profesa James Mdoe kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia umetupa faraja.



Tunawashukuru: Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Jaji (Mstaafu) Damian Lubuva, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Profesa William Anangisye, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Ndugu Nicholas Kuhanga, ambaye amewahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Profesa Rwekaza Mukandala, aliyechukua nafasi ya Profesa Luhanga kama Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na uongozi wote na jumuiya ya Chuo Kikuu kwa kumuaga Profesa Luhanga kwa heshima anayostahili.

Tunawashukuru pia Chuo Kikuu cha Mzumbe, ambako Matthew alikuwa Mwenyekiti wa Baraza. Chuo hicho kimemuaga Profesa Luhanga vilivyo.

Tunamshukuru Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Mkuu wa Chuo, Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilibahatika kufanya kazi chini yake nikiwa Waziri wa Nchi (Mazingira), Ofisi ya Makamu wa Rais; Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafe Barnabas Samatta, laiyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu.

Profesa Lughano Kusiluka, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu, na jumuiya yote ya Chuo Kikuu Mzumbe. Chuo Kikuu Mzumbe, tunawashukuru sana kwa kuchangia jeneza, gharama za kaburi na nyinginezo.

Tunatambua pia uwapo wa Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na ule wa Profesa Anna Tibaijuka, aliyekuwa mbunge mwenzangu na Waziri mwenzangu, ambaye amewahi pia kuwa Mkuu wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (HABITAT).

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, tunamshukuru Baba Padri Daktari Joseph Mosha, Baba Paroko wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Baba Thomas Kilewona, Paroko Msaidizi wa Parokia ya Mtakatifu Andrea Mtume Bahari Beach; Baba Timotheo Polepole, Paroko wa Parokia ya Bikira Maria wa Rozari Takatifu, Chunya Mjini; na kwaya na wanaparokia wote kwa kuongoza na kuendesha sala na misa takatifu ya maziko ya Profesa Luhanga. Asanteni sana.

Tunawashukuru pia Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (Engineers Registration Board), Chama cha Wanasayansi Tanzania (Tanzania Academy of Sciences), na Huduma za Maktaba Tanzania (Tanzania Library Services).

Tunazishukuru taasisi na wale wote mliochangia kwa hali na mali katika msiba huu ambao hatima yake ni maziko ya yule ambaye wenzetu wa Kenya wanamwita 'Mwendazake', yatakayofanyika kesho Jumanne tarehe 21, Septemba 2021 katika maka-

**INAENDELEA UK.14**

# Mradi wa kipekee kutumia michikichi Kigoma kumaliza uhaba mafuta ya kula

INATOKA UK.11

wastani fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, wakati kuna vyanzo vya uzalishaji nchini.

Anasema, mpango mpaka sasa umeshazalisha miche ya michikichi ya kisasa zaidi milioni sita kwa ushirikiano na JKT Bulombora na Gereza la Kwitanga, ambako yamekuwa yakisimamia vitalu vinavyoanzishwa na TARI Kihinga katika maeneo yao.

Dk. Mkamilo anasema TARI wameweka mkakati wa kuzalisha miche milioni tano kila mwaka, ili kufikia malengo ya miche milioni 20 katika kipindi cha miaka minne ijayo, hatua itakayofikiwa katika kipindi kifupi kuzalisha mafuta ya kula ya kutosha kitaifa.

Anafafanua lengo hilo la TARI ni kuzalisha mafuta tani 720,000 ndani ya miaka minne na kuvuka mahitaji ya mafuta ya sasa tani 570,000.

Mkuu huyo wa TARI anasema mazao hayo yanayoagizwa nje ya nchi, yanatokana na malighafi yanayopatikana nchini, ikiwamio michikichi.

### MKUU JKT

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele,anasema katika kuunga mkono kilimo cha michikichi wametenga ekari 2000 na tayari wameshapanda eneo robo, ekari 500.

Anasema mkakati huo wa serikali utaweza kusaidia kuokoa fedha zinazotumika kuagiza mafuta ya kula ugenini nje ya nchi na endapo wakulima wadogo na wakubwa wataongeza kasi ya kilimo hicho kwa miche bora ya kisasa - tenera.

Mkuu wa JKT, anasema Tanzania ina mahitaji makubwa ya mafuta ya kupikia na inalazimika kuagiza kutoka nje ya nchi na wao jeshi, wameamua kuitikia wito wa serikali kwa kushirikiana na TARI- Kihinga, wamezalisha miche ua michikichi tajwa zaidi ya 80,000 na imepandwa na kuna ziada miche 60,000 kwa walima michikichi wa vijiji vinavyokizunguka kikosi hicho.

### WAZIRI

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamisi Hamza Chilo, anasema kupitia Gereza la Kwitanga, jeshi hilo lilmejipanga kujiendesha kwa kuainisha miradi ya kimkakati, ikiwamo ulimaji michikichi.

Anasema, faida itakayotokana na zao michikichi mkoani Kigoma itawezesha kujenga shule na hospitali zitakazoendeshwa nchini, kuzisaidia jamii zinazozunguka Magereza.

Ameaonya wanajamii jirani, wanaoingia katika mashamba ya jeshi na kuchoma moto.

### WAZIRI MKUU

Waziri Mkuu Majaliwa, anaonyesha tabasamu kutoka kwa jitihada za watafiti wa TARI na mbegu mpya mkoani Kigoma, rai yake ni wananchi kuchangamkia fursa hiyo, kuingia katika kilmo cha mafuta chenye tija maradufu.

Waziri Mkuu anawataka wakulima wa zao hilo katika Mkoa wa Kigoma kuondoa kwa awamu michikichi iliyopandwa kwa mbegu ya zamani, inayochukua miaka saba.

Hafichi pongezi zake kwa a Gereza la Kwitanga, lililolima ekari 6000 za michikichi, ikichukua sura ya mradi mkubwa hata kuiwezesha kujiongezea mapato na hata kujitegemea.

Majaliwa anaiagiza Gereza Kwitanga, kuongeza uzalishaji mbegu za tenera na kuwapatia bure wana vijiji jirani nao watanue kilimo hicho kwa kutumia mbegu ya kisasa.

Waziri Mkuu amewahakikishia wakulima wanaolima mazao ya kimkakati nchini, kuwawezesha katika mchakato mzima wa kuandaa, kulima, kuvuna na kuwatafutia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Katika shamba la mchikichi kambini Bulombora JKT, anasisitiza mazao mengine ya kimkakati yapo chini ya uangalizi wa serikali, ili kuhakikisha inapatikana tija ya mkulima mmoja mmoja.

Anasema serikali imeamua kuongeza mazao ya kimkakati kufikia tisa; ikiwamo mchikichi, tumbaku, alizeti, kahawa, korosho, pamba na zabibu, lengo ni kuongeza tija katika mazao hayo kibiashara.

Majaliwa anadesema serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 470 kila mwaka kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi na serikali inaweka nguvu kuzalisha michikichi, ili fedha hizo zibaki nchini.

Kwa mujibu wa Majaliwa, mkakati uliopo ni kuifanya Tanzania nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki, kwenye uzalishaji mafuta ya kula, ikijitosheleza na ziada kuuzwa nje ya nchi.

Anawaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa Kigoma, kuorodhesha ya wakulima wote wa mchikichi, ili serikali iweze kuwasaidia kwa pembejeo, mbegu na mashine za kisasa.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Karibu Januari, uwe na uchungu



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

NILIPOSIKIA kuwa mwanasiasa kijana, Januari Makamba amerejea kwenye Baraza la Mawaziri nchini, safari hii akiwa na dhamana ya nishati, sikushangaa sana, badala yake nilishusha pumzi ya faraja.

Niliamini tu kwamba, sasa kazi katika wizara hiyo itafanyika. Kwa haraka mtu akisikia nishati, moja kwa moja akili yake hukimbilia kwenye umeme na mafuta jamii ya petroli.

Mambo haya mawili ndiyo yanasababisha maumivu ya kichwa kwa Watanzania wengi, si tu kwa bei, pia hata upatikanaji wake. Msamiati wa 'kata kata' umetamalaki sana katika nishati ya umeme.

Ni wapi ambako umeme haukatiki kwa sababu hizi na zile? Ni wapi ambako watu hawaichukii TANESCO? Si kwa mengine, bali kukatika katika kwa umeme kunakosababisha kuunguza vifaa, pia kuathiri vibaya uzalishaji mali.

Nchi kuwa na umeme wa uhakika, ni kuwa na maendeleo ya uhakika na ndiyo sababu serikali inafanya kila liwezekanalo, kuhakikisha kuwa umeme unakuwa wa uhakika wa ajili ya maendeleo ya viwanda na mambo mengine.

Mbali ya umeme, mafuta jamii ya petrol ni muhimu sana pia katika uzalishaji, ni muhimu viwandani ni muhimu pia katika usafirishaji mazao na bidhaa. Kupanda kwa bei ya mafuta hayo, ni pigo kwa watumiaji.

Ndiyo maana serikali inapoona mambo hayaendi sawa, huingilia kati na kuhakikisha kuwa yanakwekwa sawa, na uzalishaji kiuchumi unakuwa katika mstari nyoofu na mambo kuendelea.

Umeme Tanzania umekuwa si wa uhakika, kwani hukatika katika bila kutarajiwa na wakati mwingine bila hata kutolewa taarifa ya hadhari, na matokeo yake unapokatika na kurudi ghafla wakati mwingine kwa nguvu kubwa, huunguza kama si tu vifaa, bali hata majengo na kusababisha hasara kubwa.

Ukatikaji huo wakati mwingine umekuwa ukitolewa sababu dhaifu na wahusika, ikiwa ni pamoja na kunguru kutua kweye transfoma au kukanyaga nyaya na kusababisha mlipuko.

Kuna nyakati hutolewa taarifa za nguzo kuanguka kutokana na uchakavu, lakini pia miti kurefuka na kugusa nyaya za umeme. Taarifa hizo huja wakati tayari uharibifu umefanywa na ili kurekebisha huchukua saa, kama si siku kadhaa.

Unajiuliza. Walikuwa wapi kubaini tatizo kama hilo? Je,ina maana wafanyakazi wa Tanesco hawakagui maeneo yao ya huduma mpaka nguzo inadondoka kwa kuoza au miti kugusa nyaya bila ya kuonekana?

Hakuna msamiati unaofaa katika hali hiyo bali uzembe tu! Hivyo, ipo haja kwa uongozi mpya kuchukua hatua za dhati na za makusudi kuhakikisha, kuwa hali hiyo inatoweka sawia na wananchi wananufaika na nishati.

Kuna nyakati Profesa SospeterMuhongo, alipokuwa waziri mwenye dhamana na mahali hapo, alisimamia vema na kwa kweli katikakatika ikatoweka, mgawo nao ukaisha. Pia, akakuja na wazo la kuhakikisha nyaya za umeme zinachimbiwa ardhini na nguzo za saruji zinasimikwa.

Alipoondoka akaondoka nalo, hadi hivi karibuni Dk. Benard Kalemani alipoliibua hasa la nguzo za saruji, ili kuondokana na kilio cha nguzo kuoza, ingawa kasi ya usimikaji ni ya konokono.

Nina imani na Januari, kwamba atаimudu wizara hii kama alivyofanya akiwa chini ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan alipomudu kuondoa mifuko ya plastiki kwenye matumizi bila hata ya kutumia nguvu kubwa.

Ameanza kazi kwa kuahidi kuona Tanesco linakuwa shirika bora katika utendaji wake na utoaji huduma kwa jamii, akiahidi kupambana na uzembe, pia akiliwezesha kupata zana bora katika kurahisisha huduma zake.

Katika kauli zake, akasema katika kuleta mabadilikoTANESCO, ambayo yanaweza 'kula vichwa' vya baadhi ya watu, kutakuwa na 'uchungu wa kujifungua', ambao hatima yake ni furaha.

Si siri, kwamba huduma za TANESCO kwa wateja zimekuwa si za staha zikifuatana na kauli za jeuri kwa baadhi ya watumishi, ambao wamekuwa wakiwasilishiwa matatizo ya wananchi, pia ugoigoi katika kutatua matatizo.

Naamini katika maboresho hayo, itawezekana sasa hata ununuzi wa LUKU ufanywe kidigitali zaidi, ambako mteja akinunua umeme kwa simu, basi uwake moja kwa moja bila ya kuingiza tarakimu kama inavyofanyika sasa.

Kwa kifupi iwe sawa na kulipia kisimbuzi cha televisheni. Karibu sana Januari utumulikie maendeleo. Alamsiki!

# Kwaheri Profesa Matthew Luhanga

INATOKA UK.13

buri ya Kondo, Tegeta.

Profesa Luhanga ameacha mke, Columba Namkamba, na watoto watatu; Edith, Thompson na Jeremiah. Ameacha pia wajukuu wawili; Miriam na Abigaeli. Aidha Matthew na familia yake wamelea watoto na wajukuu wengi wa ndugu zao.

Sisi tumekuwa majirani na familia ya Matthew pale Tegeta/Bahari Beach kwa zaidi ya miaka 25. Ndugu Kadenge, aliyekuwa mhudumu wa familia yangu, akimwona Profesa Luhanga anaingia nyumbani kwake alikuwa ananitaarifu, "Profesa Luhanga amerudi. Ameingia nyumbani na madigrii yake", akimaanisha amebeba vitabu. Watoto na wajukuu yatumieni madigrii ya Profesa Luhanga.

Hatujaja kumlilia Matthew. Hapana. Tunasherehekea maisha ya mtu mwenye kipaji na uwezo mkubwa, aliyekuwa mcheshi na mpenda watu, aliyejaliwa busara, hekima na nidhamu ya hali ya juu na mzalendo aliyetoa mchango mkubwa kitaaluma na katika maendeleo ya elimu.

Nihitimishe kwa kusema kwamba pamoja na sifa zote hizo, Profesa Luhanga alikuwa binadamu wa kawaida tu, kama tulivyo sisi wengine. Lazima katika maisha yake amewakwaza na kuwaudhi baadhi yenu. Kwa hayo yote tunawaomba, tena kwa heshima kubwa, mumsamehe.

Raha ya Milele Umpe Ee Bwana na Mwanga wa Milele Umwangazie. Apumzike kwa Amani.

***Asanteni sana. Mbarikiwe sana.***





## H'shauri Bahi yatakiwa kasi upimaji ardhi

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, imetakiwa kuongeza kasi ya upimaji ardhi katika maeneo mbalimbali ili kujiepusha na ujenzi holela.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi wilayani humo.

Alisema kwa sasa maeneo mengi katika halmashauri hiyo yamepanuka kimji na kuhitaji kupangwa vizuri kwa kuzingatia taratibu za mipango miji ili kuepuka ujenzi holela.

"Kwa sasa mji wa Bahi unapanuka kwa kasi na cha msingi hapa ni kuwahi kupima maeneo na kama hakuna mpango basi mji huu utakuwa na shida na cha msingi ni kuweka nguvu katika kupanga na kupima ili usiwepo ujenzi holela," alisema.

Aliagiza kuundwa timu ya mkoa kwa ajili ya kupima takriban viwanja 8,000 ilivyokwama kwenye urasimishaji makazi holela.

"Kwa kuwa kampuni zilizokuwa zikifanya urasimishaji makazi holela Bahi zimeshindwa kukamilisha kazi kwa wakati naagiza ofisi ya ardhi mkoa kukaa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bahi iundwe na timu ya mkoa ije hapa kwa gharama ya mkurugenzi ili kukamilisha upimaji," alisema.

Aidha, aliitaka halmashauri hiyo kuangalia namna ya kuwawezesha watumishi wa umma kwa kuwapatia viwanja kwa makundi ili kununua kwa kulipa kwa awamu.

"Muwawezeshe watumishi wa umma kuwa na rasilimali ardhi kwa kuwapatia viwanja maana leo uko Bahi kesho uko eneo lingine na zipo halmashauri zimefanya hivyo lengo kumuwezesha mtumishi kupitia sekta ya ardhi kumiliki na kupata makazi," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa wilaya hiyo, Mwanahamisi Munkunda, alishukuru uamuzi wa kuagiza kuundwa kwa timu ya mkoa kwa ajili ya kukamilisha upimaji wa zoezi la urasimishaji.

Aliomba eneo la Zanka katika wilaya hiyo nalo kufanyiwa upimaji katika viwanja 181 na kati ya hivyo ni 17 pekee vilivyopimwa huku eneo hilo kwa sasa likikua kwa kasi.

"Eneo la Zanka ni muhimu ambalo baadhi ya maeneo yake yameanza kuingia kwenye migogoro ikiwamo ya kuuziana mara mbili haliwezi kuachwa bila ya kupimwa," alisema.

# Simbachawene asema Katiba iliyopo ina ubora

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema Katiba iliyopo bado ina ubora wa hali ya juu na imeleta maendeleo makubwa nchini.

Akizungumza na mamia ya wananchi wa Kijiji cha Makose na Chogola jimboni kwake Kibakwe, Waziri Simbachawene, alisema uimara wa Katiba ya Tanzania umeleta amani, kupendana, kushirikiana na kuwapo kwa kasi ya maendeleo nchini.

"Hakuna umuhimu wa kuwapo kwa mchakato wa Katiba mpya kwasasa, na vyama vya upinzani wanaitaka si kwa ajili ya wananchi bali kwa malengo yao binafsi."

"Unakuta mtu anaisema Katiba mbaya kwa kipengele kimoja tu cha Tume ya Uchaguzi, baasi, lakini Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo iliyotuweka katika hali ya kupendana, nchi ya amani, Katiba hii ya Tanzania ndiyo inayopelekea Watanzania wanamiliki rasilimali na maliasili kwa umoja bila kuwa na ugomvi, nchi nyingine kila siku wanapigana mapanga kwasababu rasilimali za nchi zao zimewekwa katika mazingira ambayo Katiba yake haijaweka vizuri na watu wanagombana kila kukicha," alisema Simbachawene.

Alibainisha kuwa Katiba ya Tanzania ni nzuri na hakuna kitu ambacho hakikosi upungufu ambao unapaswa kushughulikiwa na siyo kwa kuibomoa Katiba yote.

"Shida ya Watanzania sio Katiba mpya, ila shida ni yawanaotaka madaraka kwa njia nyepesi ndiyo shida yao wanaona ni Katiba, shida ni ya watu wachache tu kwa malengo, kwa ubinafsi wao, lakini Tanzania hakuna shida ya Katiba maana ni nzuri na imetupitisha katika vipindi muhimu na vigumu na ingesababisha nchi iweze kuvunjika," alisema Simbachawene.

Akizungumzia masuala ya jimboni kwake, aliagiza wananchi na viongozi wa kata na vijiji kulinda misitu na kuwachukulia hatua kali wanaokata miti.

"Nipo tayari nikose kura zao kwa wale ambao wanasababisha uharibifu wa mazingira, jamani kutunza mazingira ni muhimu, lazima mlijue hili, msifanye mzaha, mazingira yetu yanaharibika kutokana na wachache ambao wanalima na kukata miti kwa ajili ya kuchoma mikaa na shughuli zingine sio halali, jambo ambalo linaharibu mazingira yetu," alisema Simbachawene.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa nne kushoto), akipokea msaada wa viti na meza 100 vyenye thamani ya Sh. milioni 12 kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Jamii wa Benki ya Stanbic, Omari Mtiga (wa pili kulia), kwa ajili ya shule ya Sekondari ya Mbambala, iliyopo nje kidogo ya Jiji la Dodoma juzi. Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 22.8/- kujenga jengo Wizara ya Sanaa, Michezo

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WIZARA ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, imesaini mkataba wa ujenzi wa awamu ya pili wa jengo lake lenye ghorofa sita litakalogharimu Sh. bilioni 22.8 ambalo litajengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mji wa Serikali Mtumba.

Akizungumza jana baada ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbas, alisema jengo hilo litakuwa na ofisi za kisasa pamoja na mahitaji yote yanayohusika katika sekta za sanaa, utamaduni na michezo.

"Jengo hili litakuwa la kihistoria kwa kuwa wizara hii haijawahi kumiliki jengo la hadhi hii nzuri, matarajio yetu jengo hili litakuwa kichocheo cha sekta hizo kutoa huduma bora na stahili kwa wadau wa sekta na wananchi kwa ujumla," alisema.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha kutolewa kwa fedha hizo za ujenzi ambazo zitatolewa kulingana na taratibu za serikali na jengo linatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24 sawa na miaka miwili kuanzia sasa.

Alitaka watekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo hilo ambao ni NHC na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambao ni wasanifu na wabunifu wa majengo hayo, kukamilisha mradi huo kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, aliishukuru serikali kwa kuwaamini na kuwapa kazi ya ujenzi wa majengo ya serikali kwa kuwa waliomba na wamepewa kazi hiyo huku akiahidi kuitekeleza kwa ubora na kwa wakati kulingana na bajeti waliyopewa.

Naye, Katibu wa Kuratibu Serikali Kuhamia Dodoma, Meshack Bandawe, alisema mpango wa serikali kuhamia Dodoma umerahisisha wizara kuwa na majengo yao na zipo katika eneo moja hatua inayorahisisha wananchi kupata huduma kwa wakati.

Alifafanua kuwa majengo ya wizara yanayojengwa katika awamu ya pili yapo 24 na hadi sasa wizara nane ikiwamo ya Sanaa, Utamaduni na Michezo zimekamilisha taratibu za ujenzi huo.

Septemba 8, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa agizo kwa wizara zote zikamilishe taratibu za ujenzi wa awamu ya pili ifikapo Septemba 30, 2021.



# Wananchi wahamasishwa kutembelea vivutio utalii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya kwa kushirikiana na wadau wa utalii wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wameandaa matembezi maalum ya kutembeleza vivutio vya utalii, kwa lengo la kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa uzinduzi wa wiki ya utalii, ambapo alisema wadau watafanya matembezi hayo katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Mbeya ambako watakuwa wanahamasisha wananchi kutembelea vivutio.

Alisema wadau hao pia watatembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyoko wilayani Rungwe ambako wadau wataweka kambi ya siku moja katika eneo la Ziwa Kisiba.

Alisema katika eneo hilo kutakuwa na burudani mbalimbali zikiwamo burudani za ngoma za asili, uogeleaji kwenye ziwa hilo pamoja na kushiriki kwenye uchomaji wa nyamapori ambazo zitapelekwa katika eneo hilo.

"Katika Mkoa wetu tuna vivutio vingi sana vya utalii, tuna utalii wa vitu vya asili vikiwamo Ziwa Ngosi, Ziwa Kisiba, Fukwe za Ziwa Nyasa, kuna misitu ya asili na mapori tengefu ambayo yanavutia sana na pia tuna tamaduni zetu ambazo ni nzuri, hivyo tunawaalika watalii kuja kutembelea vivutio hivi," alisema Homera.

Alisema kilele cha Wiki ya Utalii itakuwa Jumatatu ambayo ndiyo ya kimataifa ya utalii na wadau wa utalii na uhifadhi wanafanya kazi ya kuonyesha vitu mbalimbali vya kitalii.

Mkuu wa Utalii Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Tuli Kulangwa, aliwataka Watanzania kupenda kutembelea vivutio vya ndani ili kujionea rasilimali mbalimbali ambazo nchi imejaaliwa pamoja na kujifunza mambo mbalimbali.

Aliwataka wadau wa utalii wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuongeza juhudi ya kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii ili kukuza utalii wa ndani badala ya kutegemea zaidi watalii wa nje.

Tuli ambaye ni ofisa utalii mwandamizi, alisema katika mikoa ya ukanda huo kuna vivutio vingi ambavyo baadhi havitembelewi zaidi ya watu kutokana na hamasa kuwa ndogo.

"Wiki hii nawaombeni wadau tushirikiane kuhamasisha wananchi wetu kutembelea vivutio vyetu, Watanzania tuwe na utamaduni wa kupenda vya kwetu kuna maeneo mengi tumeendelea kuboresha miundombinu ili iwe rahisi kufikika," alisema Tuli.

Nao baadhi ya wadau na waandaaji wa wiki ya utalii wa Mkoa wa Mbeya walisema wameandaa mikakati mbalimbali ya kuhamasisha watalii wa ndani ili watembelee vivutio vilivyopo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Gabriel Shawa, alisema wanakusudia kupeleka nyamapori za kutosha katika eneo la Ziwa Kisiba ili wananchi watakaopiga kambi kwenye eneo hilo wafurahie nyama hizo.

Alisema pia kwenye eneo hilo wameandaa maeneo maalum ambayo wananchi watakaotaka kulala watalala na kwamba gharama za kwenda na kurudi ni Sh. 20,000 kwa watakaokwenda na kurudi na Sh. 40,000 kwa watakaotaka kulala.

## Wajasiriamali wapewa wiki mbili kulipia vitambulisho

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuwachuwa, ameagiza ndani ya wiki mbili wajasiriamali wote wawe wamelipia vitambulisho vya ujasiriamali kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema wilaya hiyo ina wajasiriamali zaidi ya 30,000, lakini waliolipia vitambulisho na kupewa hawazidi 10,000, hivyo waliobaki wanachangia upotevu wa mapato.

Alisema baada ya wiki mbili kupita, ambao hawatakuwa na vitambulisho wataanza kutozwa ushuru kama ilivyokuwa awali kabla ya kuanzishwa kwa vitambulisho hivyo, na kwamba atakayegoma kulipa ushuru huo atachukuliwa hatua zingine.

Dk. Chuwachuwa alisema wilaya hiyo ina halmashauri mbili, lakini zote hazijafanya vizuri kwenye utoaji wa vitambulisho hivyo kwa wajasiriamali.

"Sasa ni uamuzi wa mjasiriamali mwenyewe, achukue kitambulisho cha shilingi 20,000 kwa mwaka mzima ama aendelee kutozwa ushuru kila siku... sisi tutachukua hatua za kawaida tu kwa kuanza kutoza ushuru ili mapato yasipotee," alisema Dk. Chuwachuwa.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanalipa ushuru na kulipa kodi mbalimbali ili kuiwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya afya, elimu, miundombinu ya barabara na huduma zingine za kijamii.



Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (wapili kushoto), akishirikiana na baadhi ya wananchi kumkalisha kwenye kiti mwendo, Ramadhan Mwanjelile mkazi wa Mtaa wa Hasanga, Kata ya Uyole, jijini Mbeya ambaye amepooza kwa zaidi ya miaka minne, baada ya kumkabidhi msaada kiti hicho, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dk. Tulia amwezesha aliyepooza viungo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Spika, Dk. Tulia Ackson, amemkabidhi msaada wa kiti mwendo, Ramadhan Mwanjelile, mkazi wa Mtaa wa Hasanga Kata ya Uyole jijini Mbeya ambaye amepooza ili kimsaidie kutembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Aidha, amemkabidhi Sh. 200,000 kwa ajili ya kununua kifaa maalum cha kufanyia mazoezi ya viungo ili apate nguvu kwa maelezo kuwa madaktari walimshauri anunue kifaa hicho ili kuendelea kuimarisha viungo vyake ambavyo kwa sasa havina nguvu.

Mwanjelile anadaiwa kupooza baada ya kupata ajali miaka mitano iliyopita, hali iliyomfanya asiwe na uwezo wa kufanya kazi yoyote ya kujiingizia kipato.

Akikabidhi kiti msaada huo jana, Dk. Tulia alisema alisema alipokea maombi kutoka kwa mwananchi huyo akiomba asaidiwe kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumwezesha kumudu gharama za kununua vifaa hivyo.

Alisema baada ya kupokea maombi hayo aliamua kumnunulia kiti mwendo hicho, lakini kifaa cha mazoezi hakununua kutokana na kutokuwa na taarifa mapema kwamba nacho kilikuwa kinahitajika na kwamba alijua siku hiyo wakati anakabidhi kiti mwendo.

"Sisi tumeleta kiti mwendo ili kimsaidie kutoka ndani ili angalau na yeye awe anafanya shughuli ndogo ndogo, awe na uwezo wa kutoka ndani na kwenda kuzunguka zunguka kufanya mazoezi, lakini tumepata tena maombi hapahapa kwamba anahitaji kifaa cha mazoezi hivyo tunamkabidhi fedha ili wakamtafutie," alisema Dk. Tulia.

Aliwaomba wananchi wanaomzunguka Mwanjelile kumsaidia vitu vidogo vidogo ambavyo anahitaji kwa ajili ya uendeshaji wa maisha yake ili na yeye ajisikie sehemu ya jamii, na kwamba hawatakiwi kumtenga.

Akizungumzia msaada huo, Mwanjelile alisema kiti hicho kitamsaidia kwa kuwa kabla ya kukipata hakuwa na uwezo wa kutembea, kutokana na viungo vyake kutokuwa na nguvu hasa miguu na mikono.

Alisema alishauriwa hospitalini atafute kifaa cha kufanyia mazoezi ambacho kinauzwa Sh. 170,000, lakini mpaka sasa alikuwa hajanunua kutokana na kutokuwa na uwezo na kwamba ndiyo maana aliamua kumwomba Dk. Tulia.

Alisema baada ya kupatiwa vifaa hivyo atajitahidi kufanya mazoezi ili viungo vyake viimarike na awe na uwezo wa kufanya kazi ndogondogo za kumwingizia kipato.

"Nilipata tatizo hili miaka minne iliyopita na nilipoenda hospitalini walinifanyia matibabu mbalimbali, lakini wakashauri nitafute kiti mwendo na kifaa cha mazoezi, tatizo lililokuwa limetokea ni uwezo wa kiuchumi kuwa mdogo hivyo namshukuru sana Dk. Tulia kwa msaada huu," alisema Mwanjelile.

Mama mdogo wa Mwanjelile, Tatu Mwashinga, alisema kutokana na tatizo hilo la mwanawe kupooza walikuwa wanashindwa hata kufanya kazi kutokana na kutakiwa muda mwingi kuwa naye ili kumsaidia kwa chochote anachotaka.

Alisema kwa sasa wanafamilia watakuwa na muda hata wa kufanya kazi kutokana na mwanawe huyo kuwa na uwezo wa kutembea yeye mwenyewe kwa kutumia kiti hicho.

Alisema tatizo la kupooza kwa mwanawe huyo lilitokea ghafla ambapo alianguka na kupotea nguvu kwenye viungo vya mwili na walipompeleka hospitalini alitibiwa na wataalamu wakashauri apewe kiti mwendo na kifaa cha mazoezi.



# Serikali: Karafuu haitabinafsishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, amesema zao la karafuu halitobinafsishwa kuingia katika Sekta Binafsi na kuwataka wakulima kuuza karafuu zao kupitia Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC).

Hemed Suleiman Abdalla aliyasema hayo juzi alipokuwa anaahirisha kikao cha Baraza la Wawakilishi huko Chukwani, Zanzibar.

Alisema zao la karafuu bado ni tegemeo kwa serikali katika kuingiza mapato pamoja na wakulima wenyewe kupata kipato kikubwa huku serikali ikiendelea kutoa huduma kwa wakulima wa karafuu ikiwamo mikopo nafuu ya kuendeleza kilimo hicho.

Aliyataja majukumu ya serikali kupitia wizara ya kilimo kuwa ni kuwapatia mbegu za karafuu bure zenye uwezo wa kuzalisha kwa wingi pamoja na kuwahamasisha wananchi kuanzisha vitalu vya miche.

Alisema juhudi zote hizo zinafanyika kwa lengo kuhakikisha wakulima wanaimarisha kilimo hicho kwa ajili ya kupata kipato kikubwa, hivyo hakuna sababu ya kufanya biashara ya magendo katika zao hilo.

"Ninataka niwajulishe wakulima wa karafuu kwamba serikali itaendelea kuimarisha kilimo hicho na haina nia ya kulibinafsisha zao hilo ambapo kwa upande wa wakulima watapatiwa mikopo nafuu pamoja na kuwapatia miche bure," alisema.

Aliwataka wakulima wa karafuu wanaopata ajali ya kuanguka wakati wa kuchuma karafuu, kutoa taarifa (ZSTC) ili kulipwa bima ya ajali.

Alisema utaratibu wa kulipwa fidia upo na unafahamika vizuri kwa wakulima wote wanaochuma karafuu.

Kiongozi huyo alisema katika kuondoa usumbufu wa masuala ya bima ya fidia ya ajali, ZSTC imeandaa mazingira mazuri ya kulipa fidia kwa wananchi.

"Uchumaji wa karafuu unaendelea nchini kote ambapo tunawataka wananchi wanaopata ajali wakati wakichuma karafuu kutoa taarifa katika shirika ili kulipwa bima ya ajali ambayo tumeweka mazingira mazuri na kuondoa urasimu uliokuwapo awali," alisema.

## Kampuni yatoa vifaa vya kuhifadhi taka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Biashara ya kutengeneza vifaa mbalimbali vya matumizi ya binadamu kwa kutumia taka na malighafi chakavu Tanzania (TECHNO TRADE Investiment Limited), imekabidhi vifaa kwa ajili ya kuhifadhi taka zinazotumika hospitalini na vituo vya afya Zanzibar.

Akikabidhi msaada huo jana, Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Kanali mstaafu Samuel Mjata, huko Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto mjini Zanzibar, alisema vifaa hivyo kwa ajili ya kuhifadhi mabomba ya sindano yaliyokwishatumika, vimetolewa ili kuboresha afya kwa jamii.

Alisema lengo la msaada huo ni kuimarisha vituo vya afya katika kuhifadhi mazingira na kupunguza maambukizi ya maradhi kwa binadamu.

"Kwa vile serikali ni mboreshaji mkubwa wa kuangamiza taka chafu za hospitalini, tumeona kuwa msaada huu bila shaka utaweza kusaidia katika kuhifadhi mazingira," meneja huyo alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Fatma Mrisho, alisema kutunza mazingira ni muhimu kwa jamii, hivyo msaada huo utasaidia kuimarisha hospitali kwa kuziweka katika hali iliyo bora.

Alisema vifaa hivyo vitasaidia kuondosha usumbufu wa kuhifadhi taka na kurahisisha kuziteketeza kwa kuzichoma moto ili kukinga maambukizi ya maradhi mbalimbali.

Katibu huyo aliishukuru kampuni hiyo na kuitaka kuendelea kuisaidia serikali kwa kuipatia vifaa mbalimbali vinavyotokana na malighafi kwa lengo la kutoa huduma bora kwa jamii.

Msaada huo wa maboksi 2,000 ya kuhifadhi taka, umezilenga Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja na Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania Bububu, Zanzibar.

**"Kwa vile serikali ni mboreshaji mkubwa wa kuangamiza taka chafu za hospitalini, tumeona kuwa msaada huu bila shaka utaweza kusaidia katika kuhifadhi mazingira," meneja huyo alisema.**




Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa uzinduzi wa huduma ya malipo ya serikalini (GePG) kupitia Tigo Pesa kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juzi. Kulia ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Dk. Muhsin Salim Masoud. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri aziita AZAKI kuinua uchumi nchini

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango), Jamali Kassim Ali, alisema serikali ipo tayari kufanya kazi kwa pamoja na Asasi za Kiraia (AZAKI) kwa lengo la kuona malengo endelevu yaliyowekwa ya kupambana na umaskini na kukuza uchumi yanafikiwa kikamilifu.

Alitoa kauli hiyo jana mjini Zanzibar wakati akifungua kongamano la maendeleo la AZAKI.

Waziri huyo alisema mchango wa asasi hizo katika kuyafikia maendeleo ya kiuchumi ni mkubwa na serikali amejipanga kulitekeleza hilo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejikita katika uchumi wa buluu ambao umelenga kuwekeza katika rasilimali za bahari na nishati ya mafuta pamoja na ujenzi wa bandari za kisasa, yote hayo yakitarajiwa kuzalisha ajira nyingi kwa vijana.

Alisema hatua hizo zinaendelea vizuri ambapo katika kutekeleza dhamira hiyo, serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kuelekea uchumi wa buluu kwa kuwashirikisha wadau Sekta Binafsi pamoja na washirika wa maendeleo.

"Ninapenda kuwajulisha wajumbe wa kongamano hili kwamba serikali imejipanga kutekeleza uchumi wa buluu kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ikiwamo sekta binafsi na washiriki wa maendeleo kuona tunafikia malengo ya kuleta maendeleo na kujitegemea kwa kujenga uchumi imara," alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Rukiya Wadoo, alisema malengo endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na Dira ya Maendeleo ya 2050 yanasisitiza suala la kuishirikisha Sekta Binafsi katika kuyafikia malengo ya kweli ya kukuza uchumi na kuimarisha maendeleo.

Alisema amefurahishwa na mipango mizuri iliyowekwa na Serikali ya Zanzibar kwa kuweka vipaumbele vyake katika uchumi wa buluu na rasilimali za baharini.

Alisema bado nchi nyingi zikiwamo za visiwa hazijatumia vizuri rasilimali za baharini kwa ajili ya kuwanufaisha watu wake ikiwamo uvuvi wa bahari kuu.

"Nimefurahishwa na mikakati ya serikali katika kuishirikisha Sekta Binafsi katika mipango ya kukuza uchumi na kuimarisha uwekezaji katika uchumi wa bluu," alisema.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mwamvuli wa AZAKI, Angoza Hassan Khamis, alisema uchumi wa Zanzibar utajengwa kwa ushirikiano wa serikali pamoja na washiriki wa maendeleo na AZAKI.

Alisema juhudi zinazochukuliwa na serikali kuishirikisha Sekta Binafsi kikamilifu katika mikakati yake ya uwekezaji wa uchumi wa buluu zina manufaa makubwa kiuchumi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU** KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

**VIWANJA/MASHAMBA**

**KIWANJA KINAUZWA**, KIWANJA KIPO KISUKURU JKT UKUBWA SQM 2252 KINA HATI, BEI MILIONI 60. MAWASILIANO **0786 857523 / 0655 857523.**

**Kwa Habari Motomoto**
**usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA CHETI



1164475202

**EUZEBIUS MUTAYABARWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S482/040** kilichotolewa na ILUHYA SEKONDARI mwaka 1992. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/462385/2021.**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA. 115 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**FIROZ ABDALLA WALLI**
**MWOMBAJI**
**NOOR F. WALLI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 6 Mwezi wa 10 Mwaka 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 14 Mwezi wa 9 Mwaka 2021.

NAIBU MSAJILI

116475402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA KOLEKERO**
**WILAYA YA BUKOBA**

**MADAI NAMBARI 7 YA 2021**

**Mdai: HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA**

**Anamdai**

**Mdaiwa: KIKUNDI VIJANA SELEMALA – KANYANGEREKO**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba PESA TSH. 7,200,000/=**

Kwa hiyo unahitajika/mnahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 27/09/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii inaweza kutoa kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Kuitwa shaurini kumetolewa kwa maombi ya **HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA.**
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 9/8/2021.

MAHAKAMA YA MWANZO
KOLEKERO
WILAYA YA BUKOBA

1164475102

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DODOMA DISTRICTR REGISTRY)**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO. 2 OF 2021**

**In the matter of the late MICHAEL DAWFOUD MAPUNDA of Kilimani Area within Dodoma Region**

**AND**

**In the matter of Application for letter of P Administration by DURNFORD MICHAEL MAPUNDA AND FRANK MICHAEL MAPUNDA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 28th September,2021.
**Dated at Dodoma this 22nd day of April,2021.**

Ag- DEPUTY REGISTRAR

116474602

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.195/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DENIS SALEMA SIMBA wa MOSHI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ROBERT SALEMA SIMBA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 22/09/2021.**

PRINCIPAL
PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

116474502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

## OMBI LA URAIA WA TANZANIA



116474802

**JOHN MIRING'U MBUGUA**
**S.L.P 3127, MWANZA.**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mhe. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Kazi anayofanya ni MCHUNGAJI. Anwani ya mwajiri ni S.L.P 3127 MWANZA. Yupo nchini tangu mwaka 2009. Yeyote mwenye sababu kwanini asipewe Uraia atume taarifa kwa maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 3127, Dodoma. Kumb Na. DN. 891853.

**Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

---

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Aliyekosa ubunge achangia ujenzi zahanati

**Na Christina Mwakangale**

ALIYEKUWA mgombea ubunge wa Jimbo la Mkuranga mkoani Pwani mwaka jana, kupitia ACT-Wazalendo, Mohamed Mtambo amechangia Sh. 500,000 za ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Dondo.

Mtambo alitoa fedha hizo baada ya kuombwa na wananchi wa Kijiji cha Dondo, Tarafa ya Kisiju Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani wiki iliyopita, akiwa kwenye ziara ya kushukuru wananchi kwa kumpigia kura katika uchaguzi mkuu mwaka jana.

Alisema suala la kuchangia, kuhamasisha maendeleo lisihusishwe na itikadi zozote za kisiasa kwa sababu matatizo ya wananchi hususan suala la matibabu halichagui nani ataugua na wakati gani.

"Nimekuja hapa kuwashukuru kwa kunipigia kura mwaka jana, nimeona si haki kuwakimbia kwa kuwa hatukushinda, nialikeni kwa shughuli zozote za kijamii zikiwamo hitima, harusi, hata kuchimba mitaro ya ujenzi wa zahanati yetu nitakuja.

"Uzalendo kama lilivyo jina la chama chetu ni pamoja na kurudi kutoa shukrani, kuishi na watu kidugu, kuwaunganisha na si kuwagawa," alisema Mtambo.

Awali, akitoa kero na vikwazo vya ukosefu wa huduma za afya kijijini hapo, Maganga Lugutu, alisema licha ya wananchi kujua umuhimu wa kuwa na zahanati, hali ngumu ya uchumi waliyonayo inawakwamisha kufikia lengo hilo.

"Changamoto kubwa tuliyo nayo kwa sasa ni kukosa huduma ya matibabu, mtu akiugua ni kazi kubwa kuweza kufika hospitali, kwa mfano umbali wa kutoka hapa Dondo hadi Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga kwa usafiri wa pikipiki ni Sh. 10,000 kwenda tu, bado dawa, vipimo.

Akipokea sehemu ya mchango huo kwa niaba ya Kamati ya ujenzi wa zahanati hiyo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Dondo, Kata ya Dondo wilayani humo, Omary Seif Matope, alisema kata hiyo haijawahi kuwa na zahanati tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961.

Alisema licha ya kata hiyo kuwa na idadi kubwa ya watu, shule moja ya msingi na sekondari wamekuwa wakifuata matibabu kwenye kata zingine ambazo zipo umbali mrefu na kijiji chao. Matope alishukuru mchango huo alisema utawasaidia kwenye ujenzi.

"Hadi sasa wananchi kwa nguvu zetu tumeweza kufyatua tofari 2,800 huku mahitaji yakiwa ni tofari 10,500 hadi kukamilisha boma lote, kwa niaba ya wananchi wa Dondo namshukuru huyu kijana wetu kwa kutushika mkono ni rai yangu niombe wengine waige mfano huu wa kujitoa kwa ajili ya wengine," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Fedha wa kampuni ya madini ya OreCorp Tanzania Ltd, Hilda Chuwa (mwenye kipaza sauti), alipotembelea maonyesho ya teknolojia ya madini na uwekezaji, katika viwanja vya Bombambili, wilayani humo, mkoani Mwanza juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Kuu yatupa shauri la kikatiba la Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu imetupilia mbali bila gharama shauri la kikatiba lililofunguliwa na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (pichani chini) akilalamikia haki zake za kikatiba kukiukwa katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Jaji John Mgeta baada kupitia mapingamizi yaliyowasilishwa na Jamhuri wakitaka maombi hayo yatupwe kwa sababu yana upungufu mwingi.

Jaji Mgeta katika uamuzi wake alitupilia mbali maombi na kusema kwamba mwombaji alitakiwa kuwasilisha malalamiko yake katika Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ambako kesi inayomkabili inasikilizwa.

"Mahakama inatupilia mbali maombi bila gharama, mwombaji anaweza kuwasilisha malalamiko yake katika mahakama inayosikiliza kesi yake ya jinai," alisema Jaji Mgeta.

Mahakama ilikubaliana na hoja moja ya pingamizi kwamba maombi yana kasoro kwa kukiuka kifungu namba 4(5) na 8(2) cha Sheria ya Haki za Msingi na Utekelezaji wa Majukumu, mwombaji ana njia mbadala ya kurekebisha.

Mapingamizi mengine matatu yalitupwa, awali upande wa Jamhuri uliwasilisha mapingamizi manne ya awali wakipinga maombi ya Mbowe kuendelea kuwapo mahakamani, waliomba yatupwe.



Akimwakilisha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Wakili wa Serikali Mkuu, Hangi Chang'a, alidai wanapinga jinsi maombi yalivyoletwa, upungufu wa kisheria mkubwa, sheria kukiukwa, na kuomba mahakama iyatupe, hayana msingi.

Upande wa Serikali unadai maombi yana kasoro kwa kukiuka kifungu cha 4 (5) na 8 (2) cha Sheria ya Haki za Msingi na Utekelezaji wa Majukumu, mwombaji ana njia mbadala ya kurekebisha.

Mbowe kupitia Wakili Peter Kibatala anapinga ukiukwaji wa haki zake za kikatiba.

Shauri hilo la kikatiba lilikuwa lisikilizwe mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji John Mgeta, Steven Magoiga na Jaji Leila Mgonya.

Mbowe anaiomba Mahakama itamke kwamba kuna ukiukwaji wa haki zake za kikatiba katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Amefungua maombi dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akidai wamevunja haki zake kikatiba kwa kushindwa kumpa nafasi ya kusikilizwa kikamilifu.

Katika maombi yake analalamikia kuvunjwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu uchumi ambayo ameshtakiwa nayo kwa makosa ya ugaidi.

Wakili Kibatala anadai kwa mujibu wa sheria hizo mtuhumiwa anataka asishikiliwe zaidi ya saa 48 Kituo cha Polisi na akifikishwa mahakamani hakimu anatakiwa kuhakikisha kaelewa mashtaka yanayomkabili.

Anadai Mbowe kashikiliwa kituo cha Oysterbay tangu Julai 21, mwaka huu hadi Julai 26 alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa ugaidi.

Katika maombi hayo anadai sheria zimevunjwa, mteja wake alikaa kituoni zaidi ya saa 48, alilazwa sakafuni bila kujali usalama wa afya yake, wamevunja haki zake za kikatiba, wamemtesa na kumdhalilisha.

Polisi wanadaiwa kuvunja haki hizo kwa kushindwa kumpa nafasi ya kumsikiliza kikamilifu, walishindwa kutoa taarifa kwa mawakili wake ama ndugu yake wa karibu.

Anadai Mbowe alipelekwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba bila kuambiwa anakwenda wapi na alipopanda kizimbani mahakama ilikiuka haki za kikatiba kwa kushindwa kumuuliza kama kaelewa mashtaka yanayomkabili.

"Alitakiwa afahamishwe mashtaka yake kiufasaha, mashtaka mazito, mahakama haijamuuliza kaelewa ama la zaidi ya kumwambia haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo," alidai Kibatala katika maombi yake.

Anadai Mbowe hakupewa hati ya mashtaka hadi Julai 27, mwaka huu mawakili wake walipokwenda nayo gerezani.

HABARI MICHEZO

# BIASHARA UNITED YAWEKA WAZI HAIWAOGOPI YANGA

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema anawaheshimu Yanga lakini kamwe hawaogopi mabingwa hao wa kihistoria katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Kagera Sugar itawakaribisha Yanga katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ambayo itachezwa Jumatano Septemba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema ratiba ya Ligi Kuu msimu huu imekaa vizuri na kwake kuanza na timu kongwe ambayo imefanya usajili wa wachezaji wakubwa kutoka mataifa mbalimbali.

Baraza alisema kikosi chake kimejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu katika ardhi yake ya Kaitaba.

Alisema ana kikosi imara licha ya baadhi ya wachezaji wake kuchelewa kujiunga na timu kwa ajili ya kufanya mazoezi ya 'Pre Season' ambayo yalihitaji kufanyika ndani ya wiki sita.

"Tumekiandaa kikosi kwa ajili ya kuingia katika mapambano ya kupata pointi tatu muhimu, ninaendelea kutoa maelekezo na kuhakikisha wote wanakuwa na 'fitness level' ya juu na kutengeneza kombinesheni na uelewano mzuri kabla ya kukutana na Yanga," alisema Baraza.

Aliongeza wamejiweka imara na tayari kuelekea mchezo huo wa fungua dimba ambao wanahitaji kupata matokeo chanya na si vinginevyo.

"Haitakuwa mechi rahisi kwao na hata kwetu, ninarudia kusema tena ninawaheshimu sana Yanga, ila waondoe fikra zao tutawaogopa kutokana na majina makubwa ya usajili wa wachezaji waliofanya," Baraza aliongeza.

Mkenya huyo alisema wachezaji wake wote wako vizuri na ameendelea kuwaimarisha kwa kuyafanyia kazi mapungufu aliyoyabaini katika mechi mbalimbali za kirafiki walizocheza.

Msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22 unatarajiwa kufunguliwa rasmi kesho kwa mechi ya Ngao ya Jamii ambayo utawakutanisha watani wa jadi, Simba na Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.



Naibu Spika Dk. Tulia Ackson (kulia), akiteta jambo na mpinzani wake katika mchezo wa drafti kwenye Kata ya Uyole jijini Mbeya juzi. Kiongozi huyo alijiunga na vijana hao kucheza drafti wakati wa ziara yake kwenye kata hiyo.
PICHA: NEBART MSOKWA

## Azam yapania makubwa Bara

Na Saada Akida

UONGOZI wa Azam FC umeweka wazi inahitaji kupata matokeo bora zaidi msimu huu baada ya kufanya usajili mzuri na kukiandaa vyema kikosi chao.

Azam FC itaanzia ugenini kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga kuwakabili wenyeji Coastal Union hapo Jumatatu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati (pichani), alisema maandalizi mazuri waliyofanya yamewajenga na kuwaimarisha wachezaji wao na wako tayari kuanza safari ya kuwania taji la Ligi Kuu msimu huu.

Kocha huyo alisema baada ya kumaliza mechi ya kimataifa waliwapa wachezaji wao mapumziko mafupi na sasa wamerejea kwa ajili ya kuanza mapambano ya msimu mpya.

"Ligi itakuwa ngumu kwa sababu timu nyingi zimejiandaa vyema, kuanzia katika usajili hata maboresho ya benchi ya ufundi, tuko vizuri kwenye maandalizi yetu msimu huu tutaingia kutafuta matokeo mazuri kwa kila mechi iwe ugenini au nyumbani," alisema kocha huyo.

Aliongeza msimu uliopita hawakuwa na matokeo mazuri kwenye uwanja wa Mkwakwani, sasa wanakwenda kurekebisha makosa yao na hatimaye kuanza vyema msimu huu.



## Geita yaifuata Namungo mapema

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Geita Gold kimeanza safari kuelekea Lindi kuwafuata wenyeji Namungo FC kwa ajili ya mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 utakaochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani humo, imeelezwa.

Geita Gold ambayo imepanda daraja msimu huu imeweka wazi inakwenda mkoani huko kwa ajili ya kuchukua pointi tatu.

Ofisa Habari wa Geita Gold, Amani Nicholaus, alisema kikosi chao kina msafara wa watu 30, kikiwa na wachezaji 23 na viongozi saba.

"Kikosi kiko mkoani Morogoro kitalala na kesho asubuhi (leo), kitaanza safari ya kuelekea Dar es Salaam, huenda tukapata mechi moja ya kirafiki dhidi ya KMC, na baada ya hapo tutaondoka kwenda Lindi kucheza dhidi ya Namungo FC," alisema kiongozi huyo.

Geita Gold ambayo inanolewa na kocha wa zamani wa Mbao FC, Azam, KMC na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije ilipanda daraja sambamba na Mbeya Kwanza ya jijini Mbeya.

Mechi zingine zitakuwa ni Mtibwa Sugar ikicheza dhidi ya Mbeya Kwanza, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, na Coastal Union ikiwa nyumbani, Mkwakwani, ikicheza dhidi ya Azam FC.

## Watunisha misuli kuchuana Des.

Na Faustine Feliciane

SHINDANO la kunyanyua vitu vizito litakaloshirikisha wanamichezo kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara limepangwa kufanyika Desemba 3, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Shindano hilo limeandaliwa kwa pamoja na Kampuni ya DCL kwa kushirikiana na Chuo cha Ustawi wa Jamii (Kitengo cha Ubunifu), pamoja na Clouds Media.

Mratibu wa shindano hilo, Fred Mwakisito alisema wazo la kuandaa shindano hilo limefanyiwa kazi kwa pamoja na taasisi hizo tatu likiwa na lengo la kuuendeleza mchezo huo.

Mwakasito alisema katika ngazi ya awali washiriki watachuana kwenye kanda na washindi wa kila kanda watakutanishwa kumpata mshindi wa Tanzania.

Mkuu wa Kitengo cha Ubunifu katika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dk. Riziki Michael, alisema shindano hilo ni matunda ya ubunifu chuoni hapo na kufanyika kwake ni mafanikio ya wazo hilo.

Shindano hilo litashirikisha watunisha misuli wanaume na wanawake, wabeba vitu vizito na walinzi, lakini kigezo kikubwa kikiwa ni afya nzuri kwa washiriki.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LACAZETTE NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Ufaransa, Alexandre Lacazette, 30, hana nia kusaini mkataba mpya klabuni hapo. Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Le10 Sport)***

### DE LIGT ANUKIA CHELSEA

CHELSEA wanataka kumsajili beki wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt, 22. ***(Mirror)***

### BASEL YAMTAKA KARIUS

KLABU ya FC Basel inafikiria kumchukua mlinda lango wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Loris Karius, 28. ***(Bild)***

### MARTINEZ HUYOOo BARCA

BARCELONA italazimika kulipa euro milioni 1.8 ili kumtoa Roberto Martinez kutoka kwenye mkataba wake na Timu ya Taifa ya Ubelgiji. ***(Sport)***

### MARTINEZ AFUNGUKA

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez, amepuuza ripoti zinazomhusisha na kutakiwa na Barcelona kama mbadala wa Mholanzi aliyekalia kuti kavu, Ronald Koeman (58). ***(Eurosport)***

### RUDIGER AGOMBEWA

KLABU ya Bayern Munich ina nia ya kutaka kumsajili beki wa Chelsea Mjerumani Antonio Rudiger, 28, lakini mchezaji huyo anataka kusaini mkataba mpya pale Stamford Bridge. ***(Bild)***

### LIVERPOOL SOKONI

LIVERPOOL wamemweka kwenye rada zao winga wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Marco Asensio, 25. ***(Fichajes)***

### LOFTUS-CHEEK AKUMBUSHWA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amedokeza kiungo wa England, Ruben Loftus-Cheek, 25, anapaswa kumvutia ili kuokoa maisha yake ya kuendelea kucheza hapo Blues. ***(Express)***

### CITY WAIGOMEA DORTMUND

MANCHESTER City wamekataa dau la pauni milioni 15 kutoka Borussia Dortmund kwa ajili ya mshambuliaji wa Uingereza, Liam Delap, 18. ***(Football Insider)***

### ARSENAL, MILAN VITANI

ARSENAL na AC Milan zinawania kumsajili winga wa Uholanzi anayechezea klabu ya Club Brugge, Noa Lang, 22. ***(Express)***

### RUSHWORTH AVUTIA

SKAUTI wa Barcelona wamemtazama mlinda mlango wa Brighton, Carl Rushworth, 20, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo kule Walsall. ***(Mirror)***

## DOND A SOKA
## MAGA A ULAYA




# LEWANDOWSKI HAFIKIRII KUONDOKA UJERUMANI

●●● Asema bado ana nafasi ya kuendelea kufanya makubwa akiwa na Bayern...

**MUNICH,** Ujerumani

STRAIKA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski anaamini anaweza kuendelea na kuboresha kiwango chake akiwa na miamba hao wa Ujerumani na hahitaji kwenda ligi nyingine yoyote kuthibitisha hilo.

Lewandowski alizungumza hivyo wakati akipokea tuzo ya kiatu cha dhahabu cha mfungaji bora wa bara wa ligi tano kubwa Ulaya kwa msimu wa mwaka 2020-21, juzi.

Lewandowski alifunga mabao 41, katika mechi 29 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na kuipiku rekodi ya Gerd Muller ambayo aliweka ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja.

**Lewandowski alifunga mabao 11 zaidi ya Lionel Messi ambaye alimaliza msimu wake wa mwisho na Barcelona akiwa na mabao 12 zaidi ya Cristiano Ronaldo naye aliyemaliza akiwa na Juventus.**

Katika dirisha lililopita alihusishwa na klabu kadhaa za Real Madrid na Chelsea, lakini Lewandowski sasa ameamua kuweka wazi atabakia na miamba hao wa Allianz Arena.

"Kwa sasa mimi ni mchezaji wa Bayern Munich, yanazungumzwa mengi na yanaandikwa mengi, mimi sijanyanyua mdomo wangu kuzungumza lolote," alisema nyota huyo wa kimataifa wa Poland.

"Sidhani kama nahitaji kwenda kwenye ligi nyingine ili nikathibitishe ubora wangu, hapana, hapa hapa nimefanya mengi na nina nafasi ya kufanya makubwa zaidi."

MECHI KALI
HOME
AWAY
DUNDALK FC
2.25 | 3.14 | 3.00
SLIGO ROVERS

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money
tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
halopesa
SEND

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 517,

# SOLSKJAER: SIJUTII KUONDOLEWA EFL



**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anatambua ilikuwa "hatari" kwa aina ya kikosi alichokichagua cha Manchester United kwenye mchezo wa Kombe la EFL, lakini ametetea uamuzi huo licha ya kufungwa na West Ham na kuondolewa kwenye mashindano hayo.

United iliwafunga wagonga nyundo hao wa London 2-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumapili iliyopita, lakini Jumatano walipoteza 1-0 kwenye mchezo wa raundi ya tatu ya EFL uliochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Bao la mapema la Manuel Lanzini ndio liliamua matokeo ya mchezo huo, huku United ikishindwa kutikisa nyavu licha ya kuwa na umiliki wa mpira wa asilimia 61 na kujaribu kupiga mashuti mara 27 langoni mwa West Ham.

Wakati kikosi cha Solskjaer kikionyesha nguvu kubwa kwenye Ligi Kuu England pamoja na Chelsea na Liverpool, kichapo hicho kimemaanisha wameondolewa kwenye moja ya makombe waliyokuwa wanayawania, huku wakiwa hawajabeba taji lolote tangu msimu wa 2016-17 walipotwaa Kombe la Ligi ya Europa.

Solskjaer alicheza kamali kwa kucheza kikosi cha wachezaji wapya akifanya mabadiliko 11, ingawa West Ham ilikuwa tofauti sana na ile iliyofungwa pale kwenye dimba la London.



# *Barca kumbakisha Dembele*

**BARCELONA,** Hispania

MIAMBA wa soka la Hispania, LaLiga, Barcelona wameripotiwa wameamua kufungua mazungumzo na nyota wao, Ousmane Dembele juu ya hatima ya mkataba wake mpya na klabu hiyo, kwa mujibu wa Marca.

Nyota huyo raia wa Ufaransa bado ameshindwa kucheza mechi yeyote ya Barcelona msimu huu kwa sababu ya changamoto ya majeruhi.

Mkataba wake wa sasa uko mbioni kufika tamati majira ya joto mwakani na kwa sasa yupo huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine.

Hata hivyo, ripoti zinasema kuwa klabu ya Barca inajiandaa kuhakikisha nyota huyo haendi popote.

Tarifa zinasema kuwa klabu inapanga kufanya mazungumzo ambayo yanatarajiwa kukamilika hadi kufikia Januari.

Dembele mwenye umri wa miaka 24, amecheza mechi 118 akiwa na Barcelona toka alipowasili akitokea kutokea Borusia Dortmund mwaka 20017, akifanikiwa kuona lango mara 30 katika michuano yote.

# RODRIGUEZ AIBUKIA LIGI YA QATAR




**LONDON,** England

NYOTA wa Everton, James Rodriguez ameripotiwa kukamilisha uhamisho wa kwenda kucheza soka nchini Qatar, kwa mujibu wa Daily Mail.

Nyota huyo wa Colombia ameripotiwa kufikia makubaliano ya kujiunga na Al Rayyan ya nchini humo, siku chache baada ya kocha wa Everton, Rafa Benitez kumwambia kuwa hayupo kwenye mipango naye. Winga huyo alijiunga na Everton miezi 12 tu iliyopita akitokea Real Madrid na msimu uliopita alionyesha kiwango cha juu sana uwanjani.

Benitez kabla ya kuanza kwa msimu huu alimwambia nyota huyo kuwa anatakiwa kutafuta timu ya kwenda kwa kuwa yeye hana mpango naye kwenye timu yake.

Kocha huyo wa zamani wa Liverpool alimwambia kwa mpango uliopo kwenye timu yake kwa sasa, hawezi kupata nafasi.

James mwenye umri wa miaka 30, alikuwa akilipwa mshahara wa kitita cha pauni 220,000 kwa wiki akiwa ndiye mchezaji alikuwa akilipwa zaidi kikosini hapo. Rodriguez aliondoka Everton wikiendi iliyopita na anaweza kusaini mkataba mpya na timu hiyo kabla ya wikiendi ijayo akiwa ni mchezaji huru.

# Eto'o autaka urais wa TFF ya Cameroon



**YOUNDE,** Cameroon

NYOTA wa zamani wa soka la Cameroon, Samuel Eto'o ametangaza kugombea urais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini mwake, kwa mujibu wa vyombo vya habari vimeripoti.

Eto'o aliripotiwa kutoa tangazo hilo Jumanne kupitia ukurasa wake rasmi wa Facebook, kwamba atawania urais wa shirikisho hilo.

Vyombo vya habari vya Cameroon vimemnuku akisema:-"Nimeamua kuchukua uamuzi huu kwa sababu ya kuipenda Cameroon na kupenda soka letu.

"Ni wakati wa kujenga upya mpira wetu," alielezea Eto'o katika taarifa yake hiyo. Eto'o anaweza kupambana na kizuizi kwa kile kinachodaiwa kuwa ana uraia pacha wa Hispania tangu wakati akicheza Barcelona.

Miongoni mwa masharti yanayotakiwa mgombea wa urais wa shirikisho la mpira wa miguu la Cameroon, ni marufuku ya kuwa na uraia pacha.

Eto'o ni kigogo wa tatu wa zamani kugombea urais wa shirikisho hilo.

Hata hivyo, bado haijulikani ikiwa kugombea kwake kutathibitishwa au la, huku uchaguzi wenyewe ukipangwa kufanyika Desemba 11, mwaka huu.



# 350,800 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/09/21 | 17:00 | Leeds vs West Ham | 2.71 | 3.57 | 2.46 |
| 02. 25/09/21 | 17:00 | Watford vs Newcastle | 2.37 | 3.32 | 3.01 |
| 03. 25/09/21 | 17:00 | Blackpool vs Barnsley | 2.52 | 3.31 | 2.66 |
| 04. 25/09/21 | 17:00 | Swansea vs Huddersfield | 2.27 | 3.26 | 3.06 |
| 05. 25/09/21 | 17:00 | Nottingham vs Millwall | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 06. 25/09/21 | 17:00 | Blackburn vs Cardiff | 2.34 | 3.24 | 2.95 |
| 07. 25/09/21 | 17:15 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.21 | 2.91 |
| 08. 25/09/21 | 18:00 | St Etienne vs Nice | 2.94 | 3.24 | 2.40 |
| 09. 26/09/21 | 15:00 | Mallorca vs Osasuna | 2.91 | 3.06 | 2.61 |
| 10. 26/09/21 | 16:00 | Southampton vs Wolverhampton | 2.57 | 3.22 | 2.82 |
| 11. 26/09/21 | 16:00 | Udinese vs Fiorentina | 2.66 | 3.31 | 2.66 |
| 12. 26/09/21 | 18:30 | Arsenal vs Tottenham | 2.41 | 3.17 | 3.07 |
| 13. 26/09/21 | 19:00 | Lazio vs Roma | 2.75 | 3.65 | 2.39 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 24 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5253 | Muang Thong Utd vs Ratchaburi | 2.24 | 3.65 | 2.95 |
| 18:00 | 5202 | FK Pohronie vs AS Trencin | 3.53 | 3.63 | 1.87 |
| 19:00 | 4198 | Gornik Leczna vs Lechia Gdansk | 3.48 | 3.33 | 1.97 |
| 19:10 | 2938 | SKN St Polten vs Amstetten | 1.91 | 3.59 | 3.40 |
| 19:30 | 2228 | Kolos Kovalivka vs Vorskla Poltava | 2.89 | 3.13 | 2.32 |
| 19:30 | 3474 | FC Liefering vs Dornbirn | 1.24 | 5.78 | 8.48 |
| 19:30 | 5756 | Blau Weiss Linz vs SV Horn | 1.52 | 4.17 | 5.04 |
| 20:00 | 2869 | HB Koge vs FC Fredericia | 4.25 | 3.63 | 1.71 |
| 20:00 | 3619 | Hallescher vs Magdeburg | 4.33 | 3.83 | 1.70 |
| 20:00 | 4066 | Altay vs Besiktas | 4.55 | 3.56 | 1.74 |
| 20:00 | 4262 | San Sebastian Reyes vs Tudelano | 1.73 | 3.29 | 4.65 |
| 20:00 | 4440 | Orgryte IS vs AFC Eskilstuna | 2.25 | 3.36 | 3.16 |
| 20:00 | 5023 | Gomel vs Dinamo Brest | 1.49 | 4.16 | 5.42 |
| 20:00 | 5329 | Kocaelispor vs Tuzlaspor | 1.94 | 3.39 | 3.53 |
| 20:00 | 5886 | FK Karlskrona vs Asarums IF FK | 1.49 | 4.40 | 6.20 |
| 20:30 | 1637 | Riffa Club vs Al Hala Muharraq | 1.65 | 3.87 | 4.36 |
| 21:00 | 1044 | Telstar vs Jong AZ Alkmaar | 2.48 | 3.60 | 2.48 |
| 21:00 | 1280 | Emmen vs Den Bosch | 1.48 | 4.31 | 5.68 |
| 21:00 | 1425 | SBV Excelsior vs Jong PSV | 1.94 | 3.51 | 3.51 |
| 21:00 | 2518 | ADO Den Haag vs Roda Kerkrade | 2.43 | 3.70 | 2.48 |
| 21:00 | 3596 | VVV Venlo vs Helmond Sport | 1.99 | 3.67 | 3.23 |
| 21:00 | 3674 | Almere City vs Dordrecht | 1.36 | 5.10 | 6.47 |
| 21:00 | 3819 | FC Oss vs FC Volendam | 3.13 | 3.92 | 1.96 |
| 21:00 | 4739 | FC Eindhoven vs NAC Breda | 2.31 | 3.66 | 2.64 |
| 21:00 | 4984 | Sporting Lisbon vs Maritimo | 1.29 | 5.16 | 9.52 |
| 21:00 | 5427 | De Graafschap vs Jong Utrecht | 1.45 | 4.70 | 5.48 |
| 21:00 | 5644 | Zalaegerszegi TE vs Paksi FC | 2.52 | 3.77 | 2.31 |
| 21:15 | 1066 | MAS Maghrib A Fes vs FUS Rabat | 2.22 | 3.05 | 3.15 |
| 21:30 | 1282 | FC Winterthur vs FC Aarau | 2.65 | 3.52 | 2.30 |
| 21:30 | 1832 | Greuther Furth vs Bayern Munchen | 18.94 | 9.97 | 1.10 |
| 21:30 | 2936 | KS Gornik Polkowice vs GKS Tychy | 2.81 | 3.39 | 2.25 |
| 21:30 | 4749 | Jagiellonia vs Lech Poznan | 4.55 | 3.78 | 1.64 |
| 21:30 | 5262 | FC Wil vs FC Schaffhausen | 2.70 | 3.47 | 2.29 |
| 21:45 | 1016 | Derry City vs Longford Town | 1.49 | 3.87 | 6.01 |
| 21:45 | 1146 | Galway United vs UCD Dublin | 1.96 | 3.35 | 3.49 |
| 21:45 | 1672 | Coventry vs Peterborough | 1.65 | 3.77 | 4.96 |
| 21:45 | 1871 | St Patricks vs Shamrock Rovers | 2.77 | 2.96 | 2.52 |
| 21:45 | 2509 | Dundalk FC vs Sligo Rovers | 2.25 | 3.14 | 3.00 |
| 21:45 | 3112 | Cabinteely vs Shelbourne | 6.00 | 4.55 | 1.41 |
| 21:45 | 3675 | Arbroath vs Kilmarnock | 3.37 | 3.32 | 2.05 |
| 21:45 | 4495 | Waterford Utd vs Drogheda Utd | 2.66 | 3.10 | 2.52 |
| 21:45 | 5224 | Bohemians FC vs Finn Harps | 1.57 | 3.68 | 5.42 |
| 21:45 | 5595 | Athlone Town vs Wexford Youths | 1.57 | 3.99 | 4.86 |
| 21:45 | 5922 | Treaty United vs Cork City | 2.38 | 3.20 | 2.76 |
| 22:00 | 3028 | Sochaux vs AJ Auxerre | 2.38 | 3.01 | 3.11 |
| 22:00 | 3697 | West Bromwich vs QPR | 1.66 | 3.90 | 4.64 |
| 22:00 | 3860 | Nancy vs Amiens | 2.47 | 3.17 | 2.82 |
| 22:00 | 4073 | Niort vs Paris FC | 3.20 | 3.11 | 2.27 |
| 22:00 | 4547 | Almeria vs Tenerife | 1.90 | 3.21 | 4.24 |
| 23:15 | 4377 | Gil Vicente vs Porto | 6.87 | 4.51 | 1.41 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Septemba 24, 2021

Nipashe



Barca yajipanga kumbakisha Dembele

UKURASA 22



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Jimson Mwanuke (kushoto) na nahodha wa timu hiyo, John Bocco, wakiwa kwenye mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# GOMES AANDAA 'SURPRISE' MPYA

**Na Faustine Feliciane**

## Ni kutokana na 'uzito' wa mchezo kesho ambao unahitaji zaidi...

ZIKIWA zimebakia saa chache kuelekea mechi ya watani wa jadi nchini, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema kikosi chake hakitacheza mfumo 'ulioonekana' wakati wakishuka dimbani kuwakabili Yanga katika mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii utakaofanyika kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema wapinzani wao wasitarajie kukutana na mfumo waliocheza katika mechi iliyopita ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya vigogo wa Afrika, TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwenye Tamasha la Simba Day.**

Gomes alisema katika mechi dhidi ya TP Mazembe hakuwa na 'shida' ya kupata matokeo na aliutumia mchezo huo kuwaangalia wachezaji wake tofauti na itakavyokuwa kwenye mtanange wa kuwania Ngao ya Jamii.

Mfaransa huyo alisema hana mashaka na kikosi chake na anaamini wachezaji wake watafanya kile atakachowaambia ili kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo wa ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Najua ni mfumo gani nitatumia, sitarajii kucheza vile tulivyocheza na Mazembe, hii ni mechi nyingine na yenye uzito mwingine, tutaingia uwanjani kwa lengo la kupata ushindi," alisema Gomes. Aliongeza kwa sasa anaendelea kukiimarisha kikosi chake kuelekea mchezo huo na mingine inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Hatujiandai kwa ajili ya mchezo wa Jumamosi tu, unajua baada ya mchezo na Yanga siku tatu baadaye tutacheza ugenini kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu na mwezi ujao tunaanza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo tunajiandaa kwa ajili ya michezo yote," alisema Gomes.

Kocha huyo alisema wamejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu timu zote zinafahamiana na zimekutana hivi karibuni kwenye michuano mbalimbali.

"Ni kama mechi ya fainali, lazima mshindi apatikane, tumejiandaa kupata matokeo mazuri ambayo yatatuweka kwenye rekodi nzuri ya msimu mpya," Gomes aliongeza.

Naye meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alisema wachezaji wote wako vizuri na kilichobakia ni kusubiri muda wa mchezo.

Rweyemamu alisema wamejiandaa kucheza kwa tahadhari hasa wakizingatia wapinzani wao wanahitaji kuanza kuchukua vikombe ambavyo wamevikosa kwa muda mrefu.

"Rekodi yetu ya misimu minne inawaumiza, tunajua hilo, lakini sisi pia tunahitaji kuendelea kufanya vizuri, ndio maana tumejipanga na tumejiandaa kuwakabili," alisema meneja huyo.

Baada ya mechi hiyo ya Ngao ya Jamii, Simba itasafiri kuelekea mkoani Mara kuwafuata Biashara United kwa ajili ya mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Karume Mjini Musoma halafu watatua jijini Dodoma kuwakabili wenyeji Dodoma Jiji FC ifikapo Oktoba Mosi, mwaka huu.

## Yanga : Hawataamini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wameimarisha benchi lake la ufundi kwa kumrejesha aliyekuwa Kocha Mkuu, Cedric Kaze, uongozi wa Yanga umetamba wako imara kuhakikisha wanashinda mechi ya kesho na kuanza kurejesha heshima ya klabu yao iliyopotea katika misimu minne mfululizo.

Kaze aliwasili nchini usiku wa kuamkia jana na anatarajiwa kuwa sehemu ya benchi la ufundi kuelekea mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii dhidi ya Simba utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili timu yao iko tayari kwa mchezo huo na Simba kwao si wapinzani wao kiuhalisia.

Bumbuli aliwataka mashabiki na wanachama wa Yanga kujiamini na kutokuwa na wasiwasi yoyote kuelekea mechi hiyo ya kufungua msimu mpya wa mwaka 2021/2022.

"Kulwa na Doto ni watu wanaotoka katika mfuko mmoja, Yanga na Simba hatukuzaliwa na baba mmoja, sisi sio watoto wa baba mmoja, alianza Yanga halafu Simba akafuata, Simba hawezi kuwa doto,... kwa sababu ametoka ubavuni kwa Yanga," alisema Bumbuli.

Hata hivyo, Yanga ilikataa kusema lolote kuhusiana na ujio wa Kaze ambaye amerejea nchini kuiongoza timu hiyo ambayo hivi karibuni iliondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Taarifa za ndani zinaeleza Kaze atakuwa msaidizi wa Nasreddine Nabi, ambaye ni raia wa Tunisia lakini pia benchi hilo likiimarishwa kwa uwepo wa Mwinyi Zahera kama Mkurugenzi wa Ufundi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >